# *Kutoa Presha*

Bwana akubariki, Ndugu.

2 Habari za jioni, marafiki. Ni majaliwa kurudi hapa tena, usiku wa leo, kwenye—kwenye mkutano huu mkubwa wa hadhara; imekuwa ni siku kuu kwetu sote, nina hakika. Nilikuwa na wakati mzuri sana asubuhi ya leo katika ushirika wa Neno la Mungu, na pamoja na watu huko chini kwenye kiamshakinywa cha wahudumu. Loo, laiti mngalikuwepo nyote. Hawakuwa na, nafikiri, nafasi kwa ajili ya watu, lakini, kuwakaribisha, lakini tulikuwa tu na ushirika mzuri, na (Asante.) wakati mzuri sana miongoni mwa ndugu.

3 Halafu leo kwa namna fulani imekuwa si—siku kwangu kuwaona tu wengi wa marafiki zangu na kuwatembelea. Nao wamekuwa wakimwona Roho Mtakatifu akifunua, na kuonyesha, na kurekebisha mambo.

4 Mtu fulani alikuwa akiniambia, inayodhaniwa kuwa ni kamba ndogo iliyowekwa hapa, ama kitu fulani, juu ya m—mtoto mchanga aliyekuwa na kichwa kilichojawa maji jana usiku aliyeombewa. Na, loo, kilikuwa ni kichwa kikubwa mno kilichojawa maji, naye alikuwa amelala pale nyuma ya pazia.

5 Tulipoingia, maskini mama . . . Nasi tukaenda kule, na kwa namna fulani ikanihuzunisha tu kuwazia juu ya maskini jamaa huyo mdogo, hana bahati, kijitoto kidogo tu, na kichwa chake kidogo kilikuwa kimevimba, mishipa mikubwa mno ikitokeza nje, na maskini kidevu chake na uso karibu mpana *hivyo*, na kichwa chake karibu *hivi*. Na kwa *namna fulani*, kupiga magoti tu pale na kuomba maombi ya imani, na kuweka mikono juu ya jamaa huyo mdogo, na kumpa changamoto ibilisi aliyefanya hiyo kazi. Nikamwambia maskini huyo mama, “Je, unaamini?”

Akaangalia juu na kusema, “Ninaamini.”

6 Nikasema, “Kuna jambo fulani lililompata huyo mtoto. Sasa, nataka ujue jambo hili, nenda nyumbani,” anaishi mbali na hapa, basi nikasema, “utakapofika nyumbani nataka ukipime kichwa cha huyu mtoto mchanga, ndipo kesho uchukue kipimo kingine, na kama huwezi kurudi, ukitume.”

7 Billy ndio kwanza aniambie dakika chache zilizopita ya kwamba waliiileta hiyo kamba, na kichwa cha mtoto huyo kilikuwa kimepungua kwa robo tatu ya inchi. Walimpeleka kwa daktari leo hii, nao wamekuwa wakimdunga sindano, naamini, kila siku, na—naye daktari alisema amepata nafuu sana hawahitaji sindano zingine. Nayo ile mishipa mikubwa iliyokuwa kichwani mwake tayari imeshuka, hakuna mshipa unaoonekana.

8 Basi inaonyesha tu ya kwamba Yeye yu hai. Ajabu sana! Nina furaha sana kwamba Yeye hujibu maombi, nina furaha sana kwa ajili ya jambo hilo. Nasi tunajua tu kwamba mtu yeyote atakayeamini, kumwamini tu Bwana, lita—litatukia, jambo lile lile, kwako.

9 Mnaona, kichwa hakina budi, kinaporudi nyuma, hakina budi kupata mahali pake kinaposinyaa. Na sasa, kama hao watu wako hapa walio na huyo mtoto mdogo, mbona, iweni tu waaminifu kwa Mungu, naye huyo mtoto mchanga atapona, sasa. Hiyo ni ishara kwamba Mungu aliyasikia maombi yetu.

10 Nami ninamshukuru Mungu, na ni—ninamshukuru Mungu kwa ajili yenu, mama na baba, na jamaa, na wote, wa huyo mtoto mdogo. Ninajua jinsi ningejisikia kama ingalikuwa ni mtoto wangu. Na mimi—mimi siwezi kumhisi wako kama vile ingekuwa kwa wangu, ningekuwa nikisema jambo baya, maana nisingeweza kuhisi hilo, bali ninamhurumia mtoto huyo kwa moyo wangu wote.

11 Tungalikuwa tu na wakati ningetaka kusema jambo fulani lililotukia wakati mmoja kuhusu hilo, ono ambalo halijawahi kutimia bado, na hata hivyo litatimia.

12 Leo niliingia kwenye chumba ambamo kulikuwa na mtu wa thamani, baba wa watoto watano wadogo, amelala akifa kwa kansa kubwa mno. Basi nilipomtazama, mimi . . . Yeye akasema, "Daktari anasema hakuna kitu kinachoweza kufanywa." Naye ana mtoto mchanga mwenye umri wa miezi michache tu, maskini mke wake amesimama pale akimwangalia, na jamaa mdogo mwenye sura nzuri, mumewe, na maskini mtoto mchanga ambaye . . . Sikuwaona, nafikiri walikuwa wamekuja kutoka mbali mahali fulani.

13 Kwa hiyo ninii tu, huna budi kuwahurumia watu hao. Ninawazia jambo hilo, watoto wadogo, watano sasa, kuwa bila baba, hiyo ni kazi ya ibilisi. Kwa hiyo sisi . . . Nikasema, "Nitakupeleka, kwa imani, kwenye chumba cha upasuaji cha Mungu, nami nitachukua Kisu cha upasuaji cha Mungu, kikali kuliko upanga ukatao kuwili, tutashuka moja kwa moja mahali huyo pepo amekaa, na kumkata kwa Neno." Nafikiri huyo mtu alienda nyumbani, alikuwa—alikuwa . . . Loo, Mungu ni mwema sana. Alikuwa ni jirani yangu, papo hapo ninapokaa.

14 Kwa hiyo sasa, kesho asubuhi, Bwana akipenda, mimepewa majaliwa juu ya wahudumu hawa wote wazuri na waalimu kuwa na somo la shule ya Jumapili. Basi Bwana akipenda, ninataka kuzungumza juu ya, asubuhi, *Kurudishwa Kwa Mti Wa Bibi-arusi.* Na kwa hiyo, kama wewe huko katika kanisa lako mwenyewe, mbona, tungefurahi kuwa nawe nje, saa tatu na nusu, ama saa yoyote ile asubuhi.

15 Halafu kesho usiku, tunamtarajia Mungu kufanya tena mambo makuu mno kuliko yote tuwezayo kufanya au kuwazia.

Kisha tunashuka kwenda kwa Ndugu Bigby, huko chini Carolina Kusini, siku mbili usiku, Jumatatu na Jumanne, na kisha kutoka hapo itatubidi kwenda basi nyumbani tupate kufika kwenye Cow Palace huko Pwani ya Magharibi, tutakapoenda tena.

16 Sasa kabla tu hatujalikaribia Neno, hebu na tumkaribie Mwandishi wake, huku tukiinamisha vichwa vyetu kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi. Nashangaa, usiku wa leo, huku vichwa vyetu vimeinamishwa, na ninatumaini mioyo yetu imeinamishwa pia katika Uwepo Wake, ni wangapi hapa ndani mlio na kitu moyoni mwenu mngetaka Mungu awakumbuke? Inua tu mkono wako juu na kusema, "Mungu, nikumbuke." Ni karibu asilimia mia moja.

17 Baba wa Mbinguni, ni vizuri sana kumjia Mungu aliye hai, tukijua ya kwamba Yeye ndiye Mshauri wetu mkuu, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele. Nasi tunakuja katika Jina Lake usiku wa leo, mbele ya Kiti cha Enzi cha neema Yake, kuombea mikono hii yote iliyoinuliwa. Chini ya mkono moyoni mwa mwanadamu Wewe ulijua kilichokuwa mle, Baba. Nayo inaonyesha wana haja na imani, la sivyo wasingeinua mikono yao, bali wanaamini, Bwana, ya kwamba Yule mkuu asiyeonekana yuko pamoja nasi. Wanaamini ya kwamba Wewe ungeuona mkono wao na kujua haja yao, nami nina hakika uliiona, Bwana, na nyuma ya haja hiyo kulikuwa na maombi, nami ninaweka yangu pamoja na yao juu ya madhabahu Yako, na kuomba, Bwana, ya kwamba Wewe utamjibu kila mmoja wao.

18 Ninawaombea wahudumu wote hapa, makusanyiko yao. Nasi tunashukuru, Bwana, kwa ajili ya shuhuda, kutokana na usiku huo mmoja wa maombi kwa ajili ya wagonjwa, walianza kuingia. Na maskini huyo mtoto mchanga, Bwana, loo, ushuhuda kwa tabibu. Kristo ndiye Tabibu mkuu, Yeye huponya magonjwa yetu yote, tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo.

19 Sasa, Baba wa Mbinguni, tunaomba ya kwamba utaendelea kuwa pamoja na familia hiyo, kuwa pamoja na wote walioombewa, na jalia wasiwe na wasiwasi wala kufadhaika, bali wangoje tu, na kukumbuka ya kwamba "Ombeni, na kisha jueni ya kwamba mtapewa," Mungu alisema hivyo, kamwe haliwezi kushindwa. Tujalie, Bwana.

Libariki Neno Lako usiku wa leo, tunapolisoma, na muktadha wa Maandiko upate kutolewa kwetu katika nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu.

20 Na tutakapoondoka usiku wa leo, kwenda kwenye makazi yetu mbalimbali na mahali pa kuishi kwa wakati huu, ninaomba ya kwamba itanenwa mtaani na kwenye magari, kama wale waliotoka Emau. Walipomwona Yesu, yale aliyofanya baada ya kufufuka, wakijua ya kwamba alifanya jambo lile lile baada ya kufufuka alilofanya kabla ya kusulubiwa, walijua ilikuwa ni

Yeye, kwa maana hakuna mtu angaliweza kufanya hivyo, nao wakasema, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu?"

21 Jalia, usiku wa leo, ya kwamba Roho Mtakatifu, Kristo aliyefufuka, atazungumza na kila moyo, na jalia afanye na kutenda mambo usiku wa leo, aliyofanya kabla ya kusulubiwa Kwake, ili Kanisa lipate hakikisho lingine kwamba amefufuka katika wafu na yu hai milele. Tunaomba hayo, katika Jina Lake. Amina.

22 Nina Maandiko mawili usiku wa leo, niani, ningetaka myazingatie, mojawapo ni Mithali, mlango wa 18, kifungu cha 10, hilo lingine ni Isaya 32:2. Basi katika Mithali, ya 18:10, ningetaka kusoma hili:

> *Jina la* B*WANA* *ni ngome imara: wenye haki huikimbilia,* wakawa *salama.*

23 Na katika Isaya, mlango wa 32 wa Isaya, na kuanzia kifungu cha kwanza na cha pili:

> *Tazama, mfalme atamiliki kwa haki,*. . . mkuu *atatawala kwa hukumu.*
>
> *Na mwanadamu atakuwa kama mahali pa kujificha na upepo, na mahali pa kujisitiri na dhoruba;* mto. . . *kama mito ya maji mahali pakavu, kama kivuli cha mwamba mkubwa katika nchi yenye uchovu.*

24 Nami ninatoa kutoka kwenye muktadha huu mdogo ambao ningetumia asubuhi ya leo kwenye kiamshakinywa cha wahudumu, muktadha mdogo tu ambao ningeninii. . . niliwazia huenda ukatusaidia sote, kwa sababu nafikiri unafaa, ninaliita: *Kutoa Presha.*

25 Nimekuwa nikiwazia kwamba, mwajua, tunaishi katika siku ambayo kuna presha nyingi sana, nami daima hujaribu kuwazia juu ya jambo fulani ambalo lingewasaidia watu wanaokuja kulisikiliza Neno. Kama nikisimama tu hapa na. . .

26 Sina ufasaha wa hotuba, mi—mimi si mtu mwenye elimu, wala sina mafunzo ya kikanisa, kwa hiyo jambo pekee ninaloweza kufanya ni kusoma na kuomba, na kufuata tu uongozi wa Roho, nikimwomba Mungu atufanyie jambo fulani ambalo lingetusaidia. Hiyo ndiyo sababu sisi sote tuko hapa usiku wa leo, sio kuonekana, bali kusaidiwa, na hilo ndilo kusudi letu, hilo ndilo kusudi la mkutano huu mkubwa, ni kuwa, ni kumsaidia mtu fulani, kufanyaa maisha kuwa rahisi kidogo.

27 Na siku hii kuu tunayoishi, ambapo kuna presha nyingi sana, kila kitu kinaonekana kujaa presha. Wakati mgumu sana, kila mtu anaharakisha upesi wawezavyo kwenda, wakishuka barabarani kwa mwendo wa maili tisini kwa saa kupitia kila eneo la spidi maalum, kama ni ishirini, wanaenda tisini kwa vyovyote vile. Hawapaswi kufanya hivyo, Wakristo hawapaswi, inawabidi kumpa Kaisari kilicho cha Kaisari; Mungu kilicho

cha Mungu. Lakini sisi hapa tunaenda, mbio tu tuwezavyo, tukiharakisha tu . . .

28 Nasi tuna wasiwasi sana, Siamini Wakristo halisi hufanya hivi, lakini wengi wao huwasha tu sigara moja baada ya nyingine. Kuna shida gani? Unafikiri hilo linakusaidia? Linakufanya tu uwe na wasiwasi zaidi, lakini unafanya hivyo. Madaktari wataandika makala, na kuyaweka kwenye ma—magazeti, na kusema, "Kansa tupu," wakiwaambia jinsi ilivyo hatari kuzivuta, na, lakini mnafanya hivyo kwa vyovyote vile. Kuna shida gani? Mnajaribu kutoa presha.

29 Tunaona watu wanakunywa pombe. Wanatoka nje, wanakimbia huku na huku, wanafanya karamu za ulevi kote, na kisha wanajaribu kuisahau kwa kunywa pombe. Nadhani wanafikiri hilo ndilo jambo wanalopaswa kufanya. Hiyo haitoi presha, hiyo hupandisha presha, kuliendea jambo baya, njia mbaya.

30 Ndipo watatoka na kufanya yote wawezayo, yawe mazuri ama mabaya, na—na dhambi, na kujaribu kujificha kutoka kwake, na—na kufikiri unafanya jambo kuu. Unajaribu kufanya nini? Unajaribu kujificha kutoka kwa kitu fulani, unajua umekosea. Hakuna mtu anayeweza kufanya mabaya pasipo kujua ya kwamba anafanya makosa. Asili yenyewe ndani yake, ingawa yeye ni mtu aliyeanguka, yeye ni mwana wa Mungu aliyeanguka, kuna kitu fulani ndani yake kinachomwambia kwamba ni makosa.

31 Hakuna mtu anayeweza kuzurura na mke wa mtu mwingine bila yeye kujua ni makosa, hakuna mwanamume anayeweza kulewa pasipo kujua ni kosa, hakuna mwanamke anayeweza kuvaa nguo za kizinifu pasipo kujua ni kosa, huwezi kufanya mambo hayo; lakini unafanya nini? Unajaribu kutoa presha, umepindika kabisa, umefungwa.

32 Kwa urahisi ni wakati wa fadhaa tunaoishi, ni—ni wakati tunaoishi, presha.

33 Nilikuwa nikizungumza, hapa si muda mrefu uliopita, nikiwa huko Afrika nikimwangalia mwana-kondoo mdogo kutoka ambako wenyeji walikuwa na zizi dogo, nao walikuwa wamemwachilia maskini jamaa huyo mdogo, naye alikuwa anakula, na mara akashikwa na wasiwasi sana, nami nikawaza, "Kwani maskini huyo jamaa ana shida gani?"

34 Lakini nilipokuwa nikitazama, asingeweza kumwona, lakini kwa mbali kulikuwa na simba mkubwa wa manyoya ya manjano, akinyemelea kupitia kwenye nyasi, alikuwa amesikia harufu ya maskini huyo mwana-kondoo naye alikuwa akimwendea. Mnaona, alikuwa tu na wasiwasi, hakujua ni kwa nini; wakati mwingine tunakiita jakamyo. Sasa, sababu ya yeye kushikwa na wasiwasi, hakumwona huyo simba, bali kitu fulani tu, alijua ya kwamba mauti yalikuwa yanaotea karibu.

35 Ulimwengu unaonekana kuwa katika hali iyo hiyo, wanajua ya kwamba kitu fulani kinakaribia, jambo fulani linakaribia kutukia, linapandisha presha, bila shaka, kwa mwenye dhambi, bali Mkristo, ambaye amefunzwa katika Neno, anapaswa kujua ya kwamba huko ni Kuja kwa Bwana. Inapaswa kujenga yubile tukufu ndani ya Mkristo, tukijua ya kwamba mwisho umekaribia.

36 Mtu fulani alisema, si muda mrefu uliopita, aliniambia, akasema, "Ndugu Branham, u—unawatisha watu unapozungumza juu ya, 'Huenda akaja katika saa ijayo.'"

37 Nikasema, "Kutisha watu gani? Si watu *Wake*." Mnaona? Hiyo ndiyo sauti kuu sana tunayoweza kutoa, hilo ndilo tunalotazamia, "Tazama, Bwana-arusi yuaja." Vema, hilo ndilo tunaloishia, hiyo ndiyo saa tunayoishia, najua hakuna kitu kingeweza kuwa kikuu kuliko saa hiyo. Lakini kwa mwenye dhambi, bila shaka, ni jambo la kutisha.

38 Nilikuwa nikizungumza wakati fulani, mimi huingia na kutoka mahali mbalimbali, nikihubiri, lakini mahali fulani hapana shaka nilitoa tamshi hili, huenda ilikuwa ni hapa, lakini wakati dhoruba inapoivamia n—nchi kame, nasi tunaweza kuhisi huo upepo baridi, tunajua ya kwamba mvua inakaribia. Inapaswa kutufanya wenye furaha kupumua, kwa sababu hewa hiyo imekuja kupitia kwa mvua, na ni tangazo tu tangulizi la mvua inayokuja.

39 Na wakati Wakristo wanapoona hili jambo likitukia linalotukia siku hizi, ni tangazo tangulizi la Kuja kwa Bwana. Tunaweza kuhisi upepo kutoka kwake, kumekaribia sana. Ni hisia ya kuburudisha jinsi gani kwa wale wasioogopa dhoruba, kuwa na mahali pa kuishi!

Naam, kunywa pombe, kujificha, huongeza presha, hakuitoi.

40 Siku chache zilizopita nilikuwa katika mji wetu, naye mchungaji wetu. . .Nimekuwa nikimtafuta, anapaswa kuwa hapa, Ndugu Neville, ndugu mzuri, tunampenda huko chini kwetu. Naye alikuwa Mmethodisti, aliyetoka kwenye shule ya Kimethodisti. Basi alinialika, yapata miaka ishirini iliyopita, huko chini kumhubiria usiku mmoja kwenye kanisa la Methodisti katika mji mmoja ulio chini yetu. Nami nikisimama pale nikihubiri na kuzungumza naye, nikarudi, nikaliambia kanisa, "Mnajua nini? Nitambatiza moja ya siku hizi, na Mungu atampa Roho Mtakatifu." Naye alifanya hivyo, sasa yeye ndiye mchungaji kule juu.

41 Hakuwa mgonjwa, alikuwa tu amechoka sana asingeweza kwenda mbele zaidi, nami nilikuwa nikijaribu kufanya matembezi yangu, na kwa hiyo, ilitokea kwamba, nilichukua baadhi ya yake. Ofisi ilipiga simu na kusema, "Pitia hospitalini, ukaulizie mwanamke *fulani-fulani*." Ndugu Neville ingembidi kuendesha gari kama maili thelathini kuteremka chini, ama,

maili ishirini kuteremka chini, maili ishirini kurudi. "Nenda ukawatembelee *fulani-na-fulani*."

42 Nikatoka nikaenda hospitalini, nao wakanipa jina la mama huyo, na ninii yake. . .mimi. . .Kasema, "Inapaswa kuwa," walifikiri, "kwenye orofa *fulani*." Hiyo ilikuwa kwenye orofa ya tatu ya hospitali hiyo, nikatoka nikaenda hospitalini nikaanza kushuka.

43 Kulikuwako na nesi amesimama pale akiwa na barakoa ndogo iliyoning'inia chini, nikasema, "Habari za jioni," wala hakusema neno. Nami nikasema, "Waweza kuniambia mahali, ikiwa mama huyu yuko mahali hapa au hayuko?" Nikasema, "Waliniambia alikuwa awe kwenye chumba 331."

Akasema, "Basi, nenda ukaangalie!"

Nikasema, "Asante. Naam, Mama." Presha.

Nikashuka humo chumbani, na kulikuwa na yapata watu wanne mle ndani, nami nikasema, "Je, Bibi *Fulani-wa-fulani* yuko hapa?"

"La, bwana, hayuko."

44 Vema, nikawazia labda walimaanisha 231, kwa hiyo nikaenda kwenye 231, ama, ninamaanisha 321, badala ya 31, hawakujua lolote kumhusu. Nikarudi juu, na kulikuwa na maskini daktari mmoja ameketi pale wakati huo, halisi. . . kama niliwahi kumwona mtu ambaye alikuwa mpana kadiri alivyokuwa mrefu, ilikuwa ni maskini jamaa huyo, naye alikuwa akiandika, nami nikajongea karibu, akaangalia juu, kwa namna fulani akaonyesha mshangao na kuangalia, nikawaza, "Afadhali nisiseme chochote." Kwa hiyo nikaenda zangu juu. Nikaona wote walikuwa na presha kwa sababu fulani.

45 Na kwa hiyo, nikawazia labda huenda ikawa kwenye orofa ya pili, badala ya ya tatu, kwa hiyo nikashuka kwenda kwenye tatu, uh, ya tatu, ama, orofa ya pili, nami nikamwendea nesi pale, ndipo nikasema, "Mama, kidogo nimechanganyikiwa, ninajaribu kuwatembelea wagonjwa, mimi ni mhudumu." Nikasema, "Waweza kuniambia kama mama huyu yuko katika. . .walisema 331, lakini labda ni 231."

Akasema, "Basi nenda kamtafute."

Nami nikasema, "Naam, Mama. Asante kwa taarifa yako."

Nikashuka nikaenda kule, nao wakasema, "La, hayupo hapa."

46 Kwa hiyo nikarudi, nami nikarudi tena, ndipo nikawazia, "Vema, nitarudi ghorofani tena." Nikarudi hadi orofa ya tatu, kisha nikaanza kushuka, nikawazia labda huyo angeweza kuwa katika, labda ilikuwa ni 320, ama—ama kitu fulani. Vema, sikuweza kupata mahali 320 ilipokuwa. Basi kwa hiyo, huyu hapa maskini daktari anashuka ukumbini akiwa na stethoskopu

zake, akizizungusha, nami nikamwendea, nikasema, "Habari za jioni, bwana." Kamwe hakusema neno. Nikasema, "Waweza kuniambia mbili, ama, 320 iko wapi?"

Akasema, "*Huku*, na *huko*."

Nikasema, "Asante kwa taarifa yako."

47 Ni kitu gani? Presha. Nikarudi chini kwenye lile dawati, na palikuwa na nesi mwingine, nikawaza, "Nitajaribu mara nyingine tena." Kidogo nilikuwa na wasiwasi kidogo wakati huo na kusitasita kidogo kuuliza, nami nikasema, "Mama, unaweza kunipa taarifa kidogo?" Nami nikapitia hayo tena pamoja naye.

Naye akasema, "Hebu kidogo, Kasisi, nitaangalia kwenye chati."

Nikawaza, "Mungu asifiwe!" Ni—nikatoa presha.

Kwa hiyo akaangalia chini, akasema, "Loo, amebadilishwa, yuko kwenye chumba *fulani-fulani*."

Nikasema, "Asante, sana."

48 Mnaona, wamejaa presha, madaktari wako hivyo, wauguzi wako hivyo; madaktari wa magonjwa ya akili wanawatibu madaktari wa magonjwa ya akili. Mnaona? Presha, kuna kasoro. Linaonekana tu kuwa ni la kigeni sana, ulimwengu mzima unaelekea vivyo *hivyo*. Madaktari wenye fadhaa wakimtibu mwenye fadhaa.

49 Lakini mnajua, katika hayo yote, madaktari hawana jibu, hospitali, matabibu, hawana jibu, maana wana wasiwasi pia. Lakini kuna Mmoja tu aliye na jibu, huyo ni Mungu, Yeye analo jibu.

50 Fadhaa siku zote imewashika watu. Katika Agano la Kale, wakati Israeli walipoingia Palestina na kuirithi hiyo nchi Yoshua alijenga nyumba zilizoitwa "nyumba ya makimbilio." Huko ndiko watu wangeweza kwenda kama walikuwa wamemwua mtu fulani, ama adui wao alikuwa akiwakimbiza, wangeweza kwenda kwenye nyumba hii, au, mji wa makimbilio, na wangeweza kusimama langoni na wangeweza kujitetea. Na sasa, kama walikuwa wamefanya jambo hili makusudi, vema, basi hapakuwapo na tumaini kwao.

51 Ni kama tu siku hizi, mwanadamu yuko kwenye mbio, naye anatoroka nini? Ana shida gani? Hana raha, anaenda tu kama mwendawazimu.

52 Na katika Agano hili la Kale, kama mtu huyu alikuwa amefanya hivi makusudi, basi hakuwa na bahati, lakini kama hakuwa amefanya makusudi, ilikuwa ni *bahati mbaya*. . . Basi kuna watu wengi sana siku hizi ambao kwa bahati mbaya, hawamaanishi kufanya mabaya, sasa, kuna tumaini kwa mtu huyo. Ukitaka. . . Kama unafanya makosa wala hutaki kufanya mabaya, kuna nafasi kwako, kuna mahali kwa ajili yako. Lakini

kama unatenda tu dhambi makusudi, wala hutaki mahali pa kukimbilia, basi hakuna kitu kwa ajili yako.

53 Wakati mtu huyu katika Agano la Kale, wauaji wake walipomfuata, nao jamaa za watu hawa walijua ya kwamba kama wangeweza kumshika wangemwua, kwa sababu sheria ilikuwa "jino kwa jino na jicho kwa jicho," kwa hiyo walikuwa na haki ya kumwua, kwa sababu alikuwa amefanya makosa, na, kama wakiwahi kumshika.

54 Bila shaka, alikuwa chini ya presha na angekimbia ayaokoe maisha yake, naye angeelekea mahali hapa, ama, mji wa makimbilio. Basi alipofika kule, na kama aliingia na alikuwa amewaambia uwongo langoni, yule aliyekuwa akimwandama angeweza kuja na kumkokota atoke madhabahuni na kumwua. Lakini wao... Yeye angeweza kujitetea, na kama hakukusudia kufanya hivyo, basi ilibidi hao waliomfukuza kusimama langoni, wasingeweza kusonga mbele zaidi.

55 Nina furaha sana, leo, kwamba kuna mahali pa makimbilio, ambapo mbio hizi zote, na mkukumkuku, na kukurukakara, tunaweza kutoa presha, na kuingia, kutoka kwa hayo yote.

56 Watu wanaogopa mabomu ya atomiki, wanaogopa cheche za mnururisho. Nilipokuwa nikiukaribia mji wenu hapa chini, hapa chini katika jimbo hili, vibao vikubwa mno, "Onyo," "Cheche za mnururisho." Kila mtu anaogopa, akijaribu kuchimba chini ardhini apate kuzitoroka. Unajua, umbali pekee unaopaswa kushuka ni kupiga tu magoti, una hakika kuzikwepa, kama uki—ukishuka tu umbali huo. Si lazima uwe fuko, kwenda chini ya ardhi, piga tu magoti yako, huo tu ndio umbali unaokubidi kwenda.

57 Sasa, lakini mtu huyu anayekuja hana budi kwanza ku—kukubali hayo makimbilio. Sasa, kama hajali kuhusu makimbilio, hakuna mahali kwa ajili yake, lakini ikiwa yuko tayari kukubali hayo makimbilio, basi kuna mahali alipowekewa.

58 Na ndivyo ilivyo siku hizi. Kama wewe ni mgonjwa, daktari anasema, "Utakufa," jambo lile lile lilisemwa kuhusu mtoto huyo mchanga, uh-huh, wengine, kansa, chochote kile, na sasa, kama huamini katika uponyaji wa Kiungu, vema, basi sijui mahali popote utakapokwenda, bali kama unaamini kuna chemchemi iliyofunguliwa, kama unaamini kuna Mahali, basi ninaweza kuwaambia palipo na Makimbilio, Nyumba ya makimbilio. Hakuna mtu anayetaka kufa, hakuna atakaye, unataka kuishi, na kuna Mahali pa makimbilio kwa ajili yako. Mungu alikuandalia Mahali, Mahali pa makimbilio ambapo unaweza kuachilia wasiwasi wako, kuachilia matatizo yako, na uwe salama.

59 Sasa, hana budi kutaka kukaa katika makimbilio haya. Sasa, anapoingia mle, yeye haninii... hapaswi kulalamika. Haimpasi

kuingia mle na kutembea huku na huku, aseme, "Loo, laiti ningalikuwa nje ya hapa." Kama akifanya hivyo, anafukuzwa.

60 Mnajua, tangu nilipoingia kwa Bwana wangu, ni—ninampenda sana sitaki kutoka nje. Mimi—mimi. . .Kuna jambo fulani kuhusu wokovu huu, kwamba tangu nilipoingia ndani Yake, Yeye ndiye Kimbilio langu, na ninapoingia ndani Yake, kamwe sijatamani kutoka. Sina malalamiko. Kama nilijua nitafukuzwa, basi ningekuwa na malalamiko. Lakini sina malalamiko.

61 Ninampenda, ninaupenda ushirika Wake, ninawapenda wale ambao wamechukua Kimbilio lile lile, ninapenda kushirikiana na hawa walio katika Kimbilio hili. Ushirika mzuri sana kwenye Neno la Mungu!

62 Lazima asitake kutoka nje, kwa kuwa huko nje atakufa, ndani yu hai. Amina. Nina furaha sana kwamba niko ndani. Loo, ni vizuri sana kuwa Humu ndani, kwa kuwa uko salama na mauti. Mauti hayawezi kukugusa katika Kristo, Yeye yu hai, na ni tukufu sana kwamba tumebatizwa katika Huo, ninashukuru sana kwa ajili yake, ubatizo katika Kimbilio.

63 Ndipo unapoingia kwenye makimbilio, yule aliyekuwa akikukimbiza, hana budi kusimama langoni, kwa sababu yule aliyekuwa akimfuata yuko salama. Kwa hiyo haidhuru anakimbia haraka jinsi gani, anapoingia kwenye hayo makimbilio anaweza tu kuketi chini na kutoa mvuke, hivyo tu, kuuachilia. Yuko salama, haimbidi kuhofu tena, yuko ndani basi, malango yamefungwa nyuma yake.

64 Nina furaha sana kwamba tunaweza kufa, na maisha yetu yamefichwa katika Kimbilio la Mungu, salama milele. Mshairi alisema:

> Nimetia nanga nafsi yangu katika mahali pa raha,
> Sitaabiri bahari zenye tufani tena;
> Tufani huenda ikapita juu ya kilindi cha dhoruba kali,
> Lakini katika Yesu mimi ni salama milele.

65 Mawimbi yanaweza kupiga, na kuduwaza, na magonjwa yanaweza kuja, mauti yanaweza kuja, ama chochote kile, bali wewe uko salama milele. Kristo, Kimbilio letu, lililotolewa na Mungu, Mahali pa usalama. Kristo ndiye Mahali pekee pa usalama kwa wale wanaotaka kuishi. Yeye pekee Ndiye aliye na Uzima wa Milele, hakuna kanisa, hakuna dhehebu, hakuna rais, hakuna mfalme, hakuna papa, hakuna askofu, hakuna mhudumu, hakuna kitu kinachoweza kukupa usalama ila Yesu Kristo, Yeye ndiye Mahali pekee panapoweza kukupa usalama, na Yeye ndiye Usalama uliotolewa na Mungu.

66 Loo, tunaweza kutoa *hiki* na kutoa *kile*, nacho kitaanguka, bali Mungu anapotoa chochote ni cha Milele. Na hiyo ndiyo njia

iliyotolewa na Mungu kwa ajili ya usalama wetu: katika Kristo. Ninaipenda. Unapokuwa ndani Yake, wakati shida zinapokuja, kama vile ugonjwa, au wasiwasi, masikitiko, "Alichukua huzuni zetu, kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Kila kitu tunachohitaji kwa ajili ya safari iliyosalia kiko papa hapa katika Kimbilio.

67 Tunaingiaje katika Kimbilio hili? "Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa katika Kimbilio hili," nasi tunakuwa washiriki wa Kimbilio hili. Sisi ni raia wa Ufalme huu pamoja na Mpaji wetu mkuu pamoja nasi, ambaye hutoa yote tunayohitaji. Tuamini tu Neno Lake, nasi, wakati tukiwa Humu ndani, tuko katika Uwepo Wake; ninapenda hilo.

68 Sasa, haitubidi kuharakisha, na kuzozana, na kutenda kama walimwengu wengine; tulieni kabisa. Wakristo wana shida gani? Roho ya ulimwengu siku hizi ni fadhaa, bali hiyo si Roho ya Kristo. Je, uliwahi kumwona akisisimkwa na jambo fulani? Mtulivu tu alivyoweza kuwa, Yeye alijua mahali hasa alipokuwa amesimama. Loo, ni hakikisho lililobarikiwa jinsi gani!

69 Ni kama tu mtoto mchanga, kuweka tumaini lako Kwake, na kumwacha achukue fadhaa zako zote, kwa kuwa Yeye anakujali. Usijaribu kufanya lolote kulihusu, Yeye atafanya hivyo tayari, Yeye ameahidi atalifanya. Ni kazi Yake, mradi tu unajipumbaza nalo, vema, basi Yeye hawezi kulichukua, lakini unapoliachilia na kumwacha Yeye alichukue, Yeye atalishughulikia kwa niaba yako. Naam, bwana. Loo, napenda hilo. Ni utulivu mkamilifu jinsi gani Mkristo anapaswa kuwa nao.

70 Hebu na tuwaangalie Israeli kama mfano tu. Sasa, nilijiahidi sitakaa hapa kwa muda mrefu usiku wa leo, jukwaani, kama vile nimekuwa nikifanya. Hebu na tuwaangalie Israeli, usiku wa Pasaka huko chini Misri. Huo ulikuwa ndio usiku wa kutisha sana ambao Misri ingewahi kuona, ule usiku wa Pasaka. Malaika wa mauti alikuwa nchini, mayowe yalikuwa yakitoka kila mahali, watu mitaani wakipiga yowe, mama wakizing'oa nywele zao, mtoto wao...mtoto wao mkubwa alikuwa ndiyo kwanza afariki, mabawa makubwa meusi ya malaika wa mauti yalikuwa yakielea kote nchini.

71 Lakini Israeli wangeweza kukaa watulivu tu walivyoweza kuwa. Kwa nini? Walikuwa ni watu kama tu Wamisri, bali walikuwa wametembea katika njia ya Mungu iliyoandaliwa. Walikuwa wamekubali njia ya Mungu ya makimbilio, walikuwa wamepaka damu mlangoni. Na mradi tu walikuwa wametembea katika njia hii, maandalizi ya Mungu, haikuwabidi kuwa na wasiwasi juu ya namna yoyote ya malaika wa mauti ama chochote kile, kwa sababu walikuwa...walikuwa na ahadi ya Mungu kwamba malaika wa mauti atapita juu yao.

72 Ninaweza kumwona mvulana mdogo wakati akiangalia nje dirishani, naye anakimbia kurudi kwa baba yake, ameketi

akisoma Gombo, na kusema, “Baba, mtoto Johnny Jones huko chini mtaani, niliyecheza naye, amekufa, mama yake yuko mtaani. Nami nikaangalia, na mabawa makubwa ya mwuaji yameelekea huku!” Ninaweza kumwona maskini baba, mtulivu tu, akimwangalia huyo mwana. Naye akasema, “Baba, mimi ni mzaliwa wako wa kwanza, na nyumba yetu ndiyo inayofuata. Ungewezaje kuketi namna hiyo wakati unajua ya kwamba mimi ndiye ninayefuata?”

Ninaweza kumwona maskini huyo baba akiweka Gombo chini, anamshika mvulana huyo mdogo mkono, anaenda mlangoni, na kusema, “Unaiona hiyo damu?”

“Lakini baba, damu hiyo ina nguvu gani dhidi ya mbawa hizo kubwa, nyeusi za mauti?”

“Mwanangu, ni ahadi ya Mungu kwamba Yeye: ‘Nitakapoiona hiyo damu nitapita juu yenu.’ Jambo pekee tunalopaswa kufanya ni kuipaka.”

73 Sasa, kunaweza kuwa na pi—pipa la damu limewekwa mlangoni, na kama haijapakwa, haitafanya kazi, ilibidi ipakwe katika njia iliyotolewa na Mungu. Ndivyo ilivyo usiku wa leo. Huipaki Damu kwa kuzungumza juu yake, unapaka Damu kwa kuikubali, nayo ikifika, kwenye kizingiti cha moyo wako mwenyewe, basi uko huru.

74 Maskini huyo baba hakuogopa, ninaweza kumsikia akisema, “Mwanangu, keti tu chini, toa presha. Hakuna chochote kitakachotudhuru,” mtulivu tu awezavyo kuwa, “Aliahidi ya kwamba Yeye, atakapoiona hiyo damu, ya kwamba angepita juu.”

75 Akasema, “Nilifuata kila maagizo ambayo Neno la Bwana, lililomjia nabii, lilitwambia tutekeleze, nilifuata maagizo hayo jinsi tu nabii alivyotwambia tufanye. Nami ninajua ya kwamba Mungu yuko pamoja na nabii, kwa sababu yeye ni mtu wa Mungu, nalo Neno la Bwana huwajia manabii wetu, na kwa hiyo yeye alitwambia tuipake damu hii. Yeye alikuwa na BWANA ASEMA HIVI, nami nimelitekeleza, nami ninaliamini, nami ninatulia ndani yake.” Haleluya!

76 Huenda wakakutaka ujiunge na *hili* na ujiunge na *lile*, hilo ni sawa, lakini kwangu mimi, ninataka tu Damu ipakwe, ipakwe kulingana na maagizo. Kama utafanya tu jambo lile lile sasa, basi unaweza kuketi chini na kutoa mvuke. Naam, bwana.

77 Lakini watu wa siku hizi, wakati huu wenye mashaka, wanakimbia kutoka kanisa moja hadi lingine, dhehebu moja hadi lingine, wakiwaongoa watu, loo, jamani, kila kitu kingine. Wanafanya nini? Wanaongeza tu presha.

78 Kanisa fulani linaweza kufanya mkutano mdogo, na—naye mhubiri anakuja pale, nao wanachukua karatasi yao kutoka kwenye kanisa *hili*, na kuipeleka kwa *lile*. Mwingine anakuja,

ana mkutano mdogo wa aina nyingine, nao wanaichukua kutoka kwenye kanisa *hilo* hadi kwenye *hili* hapa, wanaibeba tu kote.

79 Kwa nini usichukue tu Damu ya Mwana-Kondoo na kuipaka jinsi Mungu alivyosema ipakwe? Ndipo haitakubidi kujipumbaza na hiyo barua, "*Hili* ni la kweli ama *lile* ni la kweli?" Mungu ni wa kweli. Na kama una Damu iliyowekwa moyoni mwako, basi uko sawa na Mungu.

80 Kuongeza presha, ni kitu gani kinachowafanya wafanye hivyo? Kwa sababu walimwacha, waliliacha Neno Lake, walikubali kanuni za imani na mambo haya yote, mafundisho ya sharti, wakaliacha Neno. "Neno la Bwana ni . . . Jina la Bwana ni Ngome imara, wenye haki huikimbilia, wakawa salama."

81 Jambo ni kwamba, hatujaribu kulikimbilia Jina la Bwana, bali tunajaribu kulikimbilia jina la kanisa, na hiyo ndiyo sababu tunalitolea jasho, lakini, na kujenga presha wakati wote, kwa sababu tuna madhehebu mapya, kitu kipya, nasi tunakiendea, na muda si muda mwajua, sote tumejengeka, wala hatujui tunakosimama.

82 Lakini, "Jina la Bwana ni Ngome imara, wenye haki huikimbilia, wakawa salama." Ni mahali pa kimbilio, hujiungi Nalo, unazaliwa ndani Yake; hulipelekei barua, unaingizwa na Roho Mtakatifu, kwa kuwa umetahiriwa kutoka kwa mambo ya ulimwengu, nayo yamekufa, nyuma yako, nanyi mmefufuka pamoja Naye katika . . . Kufufuka Kwake kama viumbe vipya katika Kristo Yesu.

83 Waliliacha Neno. Wakati unapokuwa tu unaninii, unajiunga na ka—kanisa, vema, bila shaka, unaweza kujenga presha, lakini wakati umezaliwa katika Ufalme wa Mungu, presha imekwisha.

84 Hebu tuone, loo, naam, "Jina Lake ni Mnara," Mnara mkubwa sana, wenye nguvu, Kimbilio. Mnara mzuri sana ambao tunapoingia ndani Yake, Yeye hutupa hakikisho hili: "Mwombeni Baba lolote katika Jina hili kuu la ule Mnara, mtapewa." Liangalie, ingia ndani Yake, uzaliwe ndani Yake, basi mwombe Baba lolote utakalo katika Jina hilo, na umwone Yeye akiliheshimu.

85 Ni faraja jinsi gani katika saa hii, kwamba wakati watu wa ulimwengu, washiriki wa kanisa, wakikimbia kutoka mahali hadi mahali wakijaribu kupata makimbilio, nao wanasema, vema, *huyu* atasema, "Vema, inakubidi kukariri kanuni zetu za imani," *huyu* anasema, "Huna budi kujiunga na kanisa letu," lakini kwa yule mwaminio anayeingia ndani ya Kristo kwa utulivu, na kumpokea Roho Mtakatifu, na kuangalia ahadi yenyewe ya Mungu ikidhihirishwa miongoni mwao. Haiwabidi kukimbia kutoka *hapa* hadi *pale*, wanaweza tu kutoa mvuke. Hiyo ni kweli. Wanaketi chini, yote yamekwisha, wamefaulu basi. Toa presha, kwa sababu si lazima uende mbio kutoka kanisa hadi kanisa tena kwa kuwa uko ndani Yake.

86 "Jina la Bwana ni Ngome imara, wenye haki wanapoikimbilia, wanakuwa salama." Ni Ngome ya aina gani? Ni Ngome ya makimbilio ambamo tunaweza kuingia mle, na kwamba . . . Neno, Bwana ni Neno, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu."

87 Tena, "Mkikaa ndani Yangu," ule Mnara, "Maneno Yangu yakikaa ndani yenu," sasa, hiyo ni wakati ukiwa ndani, si wakati ukiwa *huko* nje ukiangalia ndani, bali unapokuwa *Hapa* ndani ukiangalia nje. Unaona? Wakati . . . "Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakae ndani yenu, mwaweza kuomba mtakalo, nanyi mtatendewa."

88 Sasa, kama huamini hiyo ni Kweli, ingia ndani wakati mmoja upate kujua. Ingia ndani upate kuridhishwa na yale Roho Mtakatifu afanyayo, usione kosa kwake, ukitaka kurudi nje tena, ingia tu na ukae pamoja Naye.

89 Jina la Bwana, Biblia ilisema, "Na kila mfanyalo kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika Jina la Bwana." Hiyo ni kweli. Nayo Biblia ilisema, "Hakuna mnara mwingine chini ya Mbingu ambao unapaswa kuokolewa kwake," si mnara mwingine, jina, si kimbilio lingine, wala makanisa, wala madhehebu, wala mashirika. Hayo yote, vema, sina neno dhidi yao, yanafanya kazi kubwa, lakini inapofikia wokovu, hakuna jina lingine chini ya Mbingu lililotolewa, ila Jina hili kuu la Yesu Kristo.

90 Hilo halimaanishi kuliitia tu, hilo linamaanisha kuingia ndani Yake, kuwa ndani Yake. Tumebatizwa ndani Yake kwa Roho mmoja. Wakorintho wa Kwanza 12, "Sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja," ambao ni Kristo Yesu. Amina. Nalipenda. Ni ninii kuu . . . limekuwa ni jambo kuu kwangu. Basi, wakati tukiwa katika Mnara huu mkubwa, ushirika tulio nao, si ni ajabu kuwa na ushirika pamoja na Kristo? Tungeweza kuomba nini zaidi?

91 Sasa, Isaya alimwelezea kama Mwamba mkuu katika nchi yenye uchovu. Hiyo ni nchi hii, nchi yenye uchovu, ama wakati wenye uchovu. Tunaishi katika wakati wenye uchovu, wakati watu wanajaribu kuchimba mashimo chini ya nyumba yao, wanaweka tangi kubwa mle ndani.

92 Vema, hivi hamjui kama bomu la atomiki lingepata kulipua mahali hapa, vema, hiyo ingepenya sana ardhini hata ingevunja kila mfupa mwilini mwako? Na mbona, baadhi ya hayo mabomu yatalipua shimo mia moja na, ama, futi mia moja na hamsini, mia mbili, labda, kwenda chini, na kuua kila kitu juu ya nchi kwa—kwa maili mia moja na hamsini, mia mbili kulizunguka. Ilipue shimo lenye kina cha futi mia mbili ama mia tatu, labda, na—na kwa maili mia moja kuzunguka, ichukue kila kitu na kukifanya majivu ya volkeno. Kama ungalikuwa moja kwa moja katikati ya dunia, katika hiyo volkeno, ingali ingekuua.

93 Hakuna njia ya kuepukia, ila juu tu, iondokee. Naam, bwana. Unapandaje juu? Shuka kwanza. Hiyo ni kweli. Vipi? Shuka, ungama dhambi zako, mwamini Bwana Yesu Kristo, ukazikwe katika ubatizo pamoja Naye, na kufufuka katika kufufuka Kwake, pamoja na Roho Mtakatifu anayekuinua juu ya masumbuko, na wasiwasi, na kutokuamini kwa ulimwengu. Naam, ndivyo hivyo. "Jina la Bwana ni Ngome imara, Mwamba wenye nguvu katika nchi ya uchovu, wenye haki huikimbilia, wakawa salama." Jinsi tunavyomshukuru Mungu kwa ajili ya jambo hilo!

94 Nilikuwa nikisoma si muda mrefu uliopita, nami ninapenda kusoma kuhusu wanyamapori; nilikuwa afisa wa uhifadhi kwa miaka mingi, nami nimewachunguza wanyamapori.

95 Karibu ninyi nyote mnajua kuhusu bu—bu—bunduki ikinilipukia, hivi majuzi, kama isingalikuwa ni Mungu, ingaliniua. Sasa, ningetaka tu kusema jambo fulani kuhusu hilo. Hiyo ilikuwa presha kubwa kupita kiasi, hiyo ndiyo iliyolisababisha.

96 Hebu niwape somo dogo hapa. Mnajua, bunduki hiyo haikuwa bunduki asili ya Weatherby. Kama nilivyosema ya kwamba nilikuwa na marafiki wangelininunulia moja, sikuzote nilitaka moja, lakini ni—ni—nisingewaruhusu kufanya hivyo kwa sababu ina bei kubwa kuliko bunduki nyingine yoyote. Basi mfanyabiashara mzuri Mkristo akampa mvulana wangu Winchester mtindo 70, naye Billy hutumia mkono wa kushoto, nao ikiwa na komeo la mkono wa kulia, wala asingeweza kuitumia. Kwa hiyo nikampa maskini Savage yangu ya .300, nami nikaichukua bunduki yake, maana nilitumia mkono wa kulia. Na kwa hiyo basi, ilikuwa ni Roberts .257, kwenu ninyi ndugu mnaobeba bunduki na kuzijua.

97 Ndipo basi ra—rafiki yangu akaja, akasema, "Ndugu Branham, kamwe usingeturuhusu kukununulia Weatherby. Sasa, Weatherby wanaweza kuitoboa hiyo, na kuifanya Weatherby kwa pesa kidogo tu, itakugharimu dola thelathini, inigharimu kama kumi ama kumi na tano." Kasema, "Acha waitoboe, hebu nikufanyie."

98 Vema, yeye ni ndugu mzuri sana, nikasema, "Endelea, ichukue." Vema, akaenda na kuitoboa. Nilipoitia risasi, na kuifyatua, nusura iniue.

99 Sasa, jambo ndilo hili: Kama hiyo ingalikuwa ni Weatherby Magnum kwanza kabisa, kamwe isingalililipuka. Kwa nini? Hiyo, hapo mwanzo, ingalianzia kwa vipande hivyo, kwa kweli ingekuwa ni Weatherby Magnum, lakini kwa kuwa ilikuwa ni kitu kingine, na kujaribu kufanya kitu fulani kutoka kwake ambacho haikuwa, ililipuka.

100 Na hiyo ndiyo shida ya Wakristo siku hizi. Hiyo ni kweli kabisa. Wapo watu wengi sana wanaojaribu kuiga Ukristo,

wanasisimkwa, wanatoka na kujaribu kutenda kama Mkristo. Ni kitu gani kinachotukia? Presha ndogo ya kwanza inapokuja, unalipuka.

101 Lakini kama ungalirudi nyuma mwanzoni na kuzaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, unaweza kustahimili presha, kwa sababu ilitumwa kwako. Hiyo ni kweli. Huna budi kuanzia mautini kuingia Uzimani, huna budi kufa, uingie kwenye lundo la takataka, ukafinyangwe tena, usipofanya hivyo, utalipukia mahali fulani.

102 Nilikuwa nikisoma hapa si muda mrefu uliopita, nilihubiri somo lililoitwa *Tai Ataharakishavyo Kiota Chake*, huko Chicago, nami nilikuwa nikisoma kuhusu aina *fulani* ya tai. Kuna aina arobaini mbalimbali zao, wanadai, linamaanisha "mraruaji kwa mdomo." Mungu daima huwafananisha watu Wake na tai, Yeye hujiita Mwenyewe Yehova-Tai, na watoto Wake wa tai, hao ni wale waliozaliwa Naye; nami nikatoa mfano mdogo fidhuli mara nyingi juu ya hilo, jinsi ambavyo, jinsi tai anavyowatayarisha watoto wake kuruka, na kuwapeleka hewani, kisha anawaachilia.

103 Na kama kunguru akijaribu kupanda kule juu, kila unyoya ungemtoka, hajashinikizwa kwake, mnaona, asingeweza kuistahimili hiyo presha. Lakini tai ndiye ndege pekee anayezaliwa na unyoya wa aina hiyo, ambaye anaweza kwenda juu sana hata mwewe asingeweza kumkaribia. Naye ana macho, na jinsi unavyozidi kwenda juu ndivyo unavyoweza kuona mbali. Basi ingemfaa nini kwenda kule juu, kama hakuwa na macho ya kuona mbali sana? Asingeweza kuona nyuma alikotoka.

104 Na hivyo ndivyo ilivyo kwa Mkristo. Baadhi ya watu labda wana tabia ya mwewe, wakila vitu vya ulimwengu, na koho, na kujaribu kuruka huko juu pamoja na tai, mbona, yeye—yeye hulipuka, kuna presha nyingi kupita kiasi, huna budi kuumbwa kwa ajili yake.

105 Basi tai wa aina hii *fulani*, anapoanza kuzeeka, anachoka, kama sisi sote wazee, naye anapata gamba kichwani mwake, ndipo anachoka sana asijue la kufanya. Na sasa, Biblia ilisema ya kwamba tai huufanya upya ujana wake, kwa hiyo nikachunguza kuhusu jamaa huyu. Basi anapozeeka na kudhoofika, na gamba hilo kote kichwani mwake, anaruka juu sana awezavyo mpaka anapata mwamba mkubwa, mrefu. Anaketi kando ya mwamba huu, naye anaketi hapo na kukigongesha kichwa chake juu ya mwamba huu.

106 Anajaribu kufanya nini? Kugonga na kuondolea mbali gamba, gamba lote. Nayo damu itaruka kutoka kichwani mwake, anapitia kila namna ya mateso. Lakini mradi tu anaweza kuhisi baadhi ya gamba juu yake, hana budi kuliondoa

hilo, kwa hiyo analigongesha kwenye mwamba, anaendelea tu kuligongesha mpaka gamba lote limetoka kichwani mwake.

107 Na mara tu gamba lake lote likitoka kichwani mwake, ingawa anatokwa na damu, amejeruhiwa, yeye hulia tu kwa sauti yake yote, anatoa presha. Kwa nini? Kwa sababu, mara tu gamba hilo lote likitoweka, basi anaufanya upya ujana wake, hakika utakuja, kwa hiyo yeye, mara tu gamba lote limekwisha, anaweza kuanza kupiga mayowe, kwa sababu anajua ya kwamba ameondoa gamba lote. Kwa hiyo ujana wake hakika utafanywa upya, kwa hiyo anaweza tu kutoa presha, aanze kupiga mayowe, kwa sababu anarudi kuwa tai kijana tena. Hilo ni zuri sana. Nina furaha kwa ajili ya huyo tai, nina furaha kwa ajili ya ndege huyo.

108 Lakini unajua, ninajua Mwamba ambapo tunaweza kwenda, na kugongesha katika maombi mpaka gamba lote la ulimwengu limepondwa likaondolewa kwetu, mpaka kutokuamini kote katika Neno la Mungu kunaondolewa, mpaka tuingie mahali ambapo mambo yote yanawezekana. Na mara tu tunapougongesha ulimwengu wote na kutokuamini Neno la Mungu kukatuondokea, basi tunaweza kupiga mayowe na kupaza sauti kwa sababu Uzima wa Milele ni wa hakika, hakika tu kama chochote kile. Bila shaka, kwa sababu ulimwengu wote umegongeshwa ukaondolewa.

109 Ukiudumisha ulimwengu kwako, ukiendelea kuupenda ulimwengu na mambo ya ulimwengu, hakika utakufa, lakini kama unaweza kuepuka hayo yote, basi ujana wako utarudishwa, utakuwa na Uzima wa Milele; nina furaha sana kwa jambo hilo.

110 Nilikuwa nikisoma wakati fulani kuhusu lile Tangazo la Ukombozi, wakati watumwa, ndugu weusi, dada huko kusini, wakati walipokuwa na utumwa. Basi wakati Tangazo la Ukombozi lilipotiwa sahihi (Walikuwa wamecharazwa, na kupigwa, na kadhalika, na walikuwa watumwa, nasi tunajua kilichotukia.), walisema, "Asubuhi *fulani*," siikumbuki hiyo tarehe sasa hivi, lakini, "hiyo ndiyo asubuhi ambayo mtakuwa huru, nanyi mtakuwa huru jua litakapochomoza. Jua litakapochomoza watumwa wote wangeweza kuwa huru."

111 Hao watumwa maskini, wanyonge, waliopigwa sana, walikuwa na hamu kuu sana ya kuwa huru, mpaka wenye nguvu kuliko wote wakapanda juu kabisa, kilele cha kilima. Wanawake na wanyonge wakashuka wakaja. Wale wasio na nguvu sana walipanda juu kidogo, na wanawake, kisha watoto. Nao wale wenye nguvu mno, walioweza kwenda mpaka juu kabisa, walisimama kule kabla ya mapambazuko, nao wakaangalia, na kuangalia, mpaka baada ya kitambo kidogo wakaanza kuona miale ya jua ikichomoza, kulikuwa kungali giza bondeni, wakapashana habari chini. Mmoja akapaza

sauti kutoka juu, "Tuko huru!" Aliyefuata akapaza sauti, "Tuko huru!" Kote mpaka chini bondeni, "Tuko huru! Jua limechomoza!" Wangeweza kutoa presha, na kupiga mayowe na kupiga makelele kwa sauti yao yote, kwa sababu walikuwa huru, jua lilikuwa limechomoza.

112 Hilo lilikuwa ni j-u-a, lakini, loo, ndugu, sasa M-w-a-n-a amechomoza. Tuko huru! Haleluya! Ishara za kufufuka Kwake ziko moja kwa moja miongoni mwetu, "Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele." Yeye hajafa, bali yu hai milele. Mwana ametokea, tunaweza kupiga makelele na kumsifu Mungu. Mwana ametokea, nasi tunaishi. Yeye yuko pamoja nasi, ndani yetu, akithibitisha Uwepo Wake kwa ishara Zake kuu za ufufuo na maajabu.

113 M-w-a-n-a ametokea, enyi watumwa wa dhambi, na madhehebu ya kanisa, ukanisa, na mambo hayo yote, mko huru. Mwana wa Mungu amefufuka akiwa na uponyaji katika mbawa Zake, naye Mwana ametokea. Nina furaha sana kwake.

114 Wakati mmoja huko Kentucky, huko juu kwenye nchi ya milimani nilikotoka, nilikuwa nikihubiri. Nami, mapema alasiri, mimi, nikihubiri juu ya kuzimu, moto, na kiberiti kwa ajili ya asiyeamini, kulikuwa na maskini mkata miti huko nyuma, nami nikasema, "Ninyi nyote walevi," naye alikuwa mmojawao, nikasema, "afadhali mtubu. Jiwekeni sawa na Mungu."

115 Kulikuwa na jamaa aliyekuja usiku uliotangulia, walikuwa wakikata mahindi, naye alikuwa na m—msumari mkubwa uliotokea kwenye ovaroli yake, akasema, "Tutapanda kule juu," nilikuwa nikihubiri kwa yapata mwaka mmoja, kasema, "tutamtupa maskini mhubiri huyo nje ya dirisha."

116 Kwa hiyo, akaja mlangoni, mtu fulani akaja akaniambia, kasema, "Hilo ndilo kundi gumu kuliko yote yaliyopo hapa." Amesimama pale, jamaa mkubwa mno, aliyeonekana mkakamavu, mikono yake imekunjwa, ndevu zimening'inia usoni mwake, yapata umri wa miaka thelathini, loo, alikuwa ni mtu mwenye sura mbaya, naye akaendelea kuniangalia, nikaendelea tu kuhubiri moja kwa moja juu ya, "Tubuni la sivyo mtaangamia!"

117 Kidogo alikaa muda mrefu kupita kiasi, Roho Mtakatifu akamshika, akaanguka sakafuni, asingeweza kufika madhabahuni upesi vya kutosha. Akaja ameweka mikono yake juu ya kichwa chake, alikuwa akilia, "Mungu, unirehemu!"

118 Usiku uliofuata mtoto wake mdogo akaketi kule nyuma, msichana wake mdogo akanipa shada dogo la maua nilipoingia mlangoni, akasema, "Ndugu Bill, tuna baba mpya nyumbani. Ninataka kukuonyesha ya kwamba ninakupenda kwa kuja hapa, na kumwacha Yesu atufanyie baba mpya."

119 Huku maskini huyu mlevi akiketi pale, nami nikasema, "Enyi walevi wote, ninyi nyote wenye dhambi, tubuni," naye akakasirika, naye akaamka akaenda nyumbani, akaenda kulala.

120 Nilikuwa nikikaa nyumbani kwa babu yangu, na kwa hiyo basi, nilipokuwa na mkutano. Na huko juu, tungeninii... unaenda kuvuka vilima wakiwa na taa mkononi mwao.

121 Na kwa hiyo wakati ninii...Yapata mwendo wa usiku wa manane maskini jamaa huyu akashuka, alikuwa akigonga mlango. Nami nikasema...nikafungua mlango. Akasema, "Ndugu Branham, nataka uniombee." Kasema, "Nilikuwa na ndoto mbaya sana muda mfupi uliopita," naye akasema, "Si—siwezi kuvumilia usiku kucha."

Nikasema, "Kuna nini?

122 Akasema, "Ni—niliota kwamba nilikuwa sungura." Naye akasema, "Nilikuwa nimeketi kondeni, nikila tu klova na kuwa na wakati mzuri, na nilikuwa nikifanya nipendavyo." Nami nikasema, "Baada ya kitambo kidogo nikasikia mbweko wa mbwa mkubwa mwindaji," kisha kasema, "huyo mbwa alikuwa amenifikia kabisa." Kisha kasema, "Nikaanza kukimbia," lakini kasema, "huyo mbwa alikuwa na mbio kuliko mimi."

123 Kisha kasema, "Ilitokea kwamba niligeuka na kuangalia, na kulikuwa na jiwe kubwa ambalo nilikuwa nimesikia habari zake." Kisha kasema, "Katika mwamba huo kulikuwa na shi—shimo," kisha kasema, "Nilijua kama ningeweza tu kuingia kwenye hilo shimo kabla ya huyo mbwa, ningekuwa salama, lakini kama nisingeweza kumtangulia, angenipata."

124 Kisha kasema, "Ndugu Branham, nilipokuwa nikikimbia kwa yote yaliyokuwa ndani yangu, nikijua dakika yoyote ningeliwa mzimamzima, maana ningeweza kuhisi pumzi ya moto ya huyo mbwa alipokuwa akiruka juu ya visigino vyangu," ndipo kasema, "mara alipofanya ule mnyakuo, niliingia kasi shimoni." Basi kasema, "Nilipoingia, niliketi chini, nikatoa presha." Jambo ndilo hilo.

125 Yeye ni Mwamba katika nchi yenye uchovu. Kuna ufa katika Mwamba kwa ajili ya wenye dhambi, kutokuamini, kimbia tu uingie kwenye Mwamba na uwe salama; Kristo ndiye Mwamba wetu. Watu siku hizi wanakimbilia kila kitu ila Kristo, wanayakimbilia madhehebu, wanakimbilia mihemuko, kila mtu ana damu, moto, moshi, ama chochote kile, na watu wanakifuatilia.

126 Kwa nini usichukue Neno Lake? Kwa kuwa Yeye ni Neno, kimbilia Hilo nawe uko salama, maana "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe." Naam, bwana.

127 Siku hizi daima ni jambo fulani linalowapasa kufanya, watakimbilia kanuni ya imani, watajiunga kisha wajitenge, na kadhalika, kutoka moja hadi lingine, bali hawatajaribu

kumchukua Kristo. Mwangalieni anapojithibitisha Mwenyewe. Hayo yote hupandisha presha, huna budi kuitoa. Liamini tu Neno Lake.

128 Ninalipataje, Ndugu Branham? Yohana Mtakatifu 5:24, Yesu alisema, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, hataingia Hukumuni; amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Hivyo ndivyo Yesu alivyosema.

129 Matendo 2:38, Petro alisema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, mtapata kimbilio, mtampokea Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ni kwa ajili yenu, na watoto wenu, na wote walio mbali, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Hapo ndipo mahali pa kuja.

130 Marko 16 ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Mnajua kile—kile kilicho ndani mle, mnajua matokeo yake ni nini. Unapofanya hivi, umepita kutoka mautini kuingia Uzimani, nawe una Uzima wa Milele, nawe unaweza kutoa presha. Kwa nini usiiachilie? Watu wamefadhaika sana, wanasumbuka sana, wanatoa tu presha. Kuna Nchi ng'ambo ya mto, kuna Kimbilio, na Kimbilio hilo ni Kristo.

131 Leo, haitubidi kushangaa juu yake, tunajua ni kweli. Mungu anapofanya ahadi katika Biblia Yake, nasi tunaiona ikitimizwa, basi tunajua ya kwamba ni kweli. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Hakuna kitu kingine kinachoweza kufanywa.

132 Sasa, unajuaje hilo, siku hizi wakati mkusanyiko mkubwa wa "Kila mtu ana *hiki*, na *kile*, *hiki* na *kile*"? Lakini, nasi tunajua ya kwamba Mungu hutoa ishara, kuna ishara barabarani. Kama hukuwa na kibao cha barabarani, usingejua unakoelekea. Huwezi kuchukua ramani ya barabarani na kuenda, isipokuwa uwe na kibao cha barabarani kuona unakoelekea. *Hii* ndiyo Ramani ya barabara, *Hii* Ndiyo inayotwambia kama tuko sahihi au la.

133 Yesu alisema, "Ishara hizi," katika Marko 16, "zitaelekeza njia." Yesu alisema katika Yohana 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya; nyingi kuliko hizi atazifanya, maana Mimi naenda kwa Baba." Hilo ndilo kimbilio. Kwa maneno mengine, kama ukiingia ndani Yake, asili Yake na Uhai Wake utakuwa ndani yako, nawe unaweza kuuhisi, unaweza kuuona, nao utazaa ule Uhai hasa ambao Biblia ilisema utazaa.

134 Kama ulinunua mmea nao ulikuwa ni mzabibu, nao huo mzabibu ukatoka na ukatoa tawi lake, nalo tawi hilo lilikuwa na zabibu, sasa, utawezaje kupata mzabibu mwingine wenye boga juu yake, na tawi lingine likitokea kwake litakuwa na kitu kingine? Kama ndivyo, ni mzabibu uliopandikizwa.

135 Na hiyo ndiyo shida siku hizi, tuna vitu vingi kupita kiasi vilivyopandikizwa vinavyoitwa “Kanisa la Kristo.” Tuna vipandikizi vingi kupita kiasi, Hilo linajishuhudia tu Lenyewe.

136 Hapa majuma machache yaliyopita nilikuwa nikizungumza kwenye matangazo ya kimataifa kwa ajili ya Wafanyabiashara wa Full Gospel huko California. Basi nilipofanya hivyo, nilikuwa nikizungumza juu ya mti ambao nilikuwa nimeuona kwenye ranchi ya Ndugu Sharrit huko Phoenix, nafikiri ulikuwa na aina tisa mbalimbali za matunda juu yake, nao ulikuwa ni mchungwa. Nami nikasema, “Nataka kukuuliza jambo fulani, Ndugu Sharrit.” Nikasema, “Sasa, kuna balungi, na kuna che—chenza, kangaja, na limau.” Loo, sijui ni michungwa mingapi iliyokuwa kwenye mti huo. Nami nikasema, “Mti huo, yalifikaje hapo?”

Akasema, “Vema, niliipandikiza, yote ni aina ya mchungwa, kwa hiyo niliipandikiza.”

137 Nikasema, “Sasa, majira yajayo ya kuchipua, ama wakati mwingine utakapozaa, kwa kuwa asili yake ni mchungwa, basi utazaa, matawi haya yote yatazaa machungwa?”

138 Akasema, “La, la. Uh-um. La. Litazaa aina ya tawi lililo ndani yake.” Kasema, “Kama ni—kama ni—kama ni tawi la limau katika mchungwa, bado, litazaa malimau.” Kisha kasema, “Kama ni—kama ni ta—tawi la chenza, litazaa machenza, likiishi kwa uhai ule ule.”

Nikasema, “Basi halitazaa machungwa tena?”

Akasema, “Loo, naam, wakati huo mti wa asili utakapotoa moja ya matawi yake ya asili, utazaa machungwa.”

Nikasema, “Mungu asifiwe, jambo ndilo hilo!”

139 Yesu alisema katika Yohana 14, “Mimi ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi.” Ndipo tawi la kwanza lililochipuka kutoka kwenye Mzabibu huo, waliandika Kitabu cha Matendo nyuma yake. Vema. Na leo hii, tuna madhehebu yanayoishi kwa jina la Ukristo, bali yanazaa tu matunda ya kimadhehebu. Hiyo ni kweli. Lakini kama Mzabibu huo ukipata kuchipusha tawi lingine, litaandika Kitabu cha Matendo nyuma yake, kwa sababu litaleta ule Uhai asilia.

140 Ikiwa Roho wa Kristo yuko ndani ya Kanisa, vema, atafanya kazi za Kristo, Yesu alisema hivyo. Ndipo tunaweza kutoa mvuke, kutoa presha. Haikubidi kukimbia kutoka kanisa hadi kanisa, njoo tu kwa Kristo.

141 Yeye alifanya nini? Tulimjuaje? Angekuwa nini kama angalikuwa hapa mjini usiku wa leo? Angefanya nini kama angalisimama hapa? Angewaambia juu ya Mahali fulani. “Msiogope . . . ” Jambo la kwanza kwenye ule ufufuo, “Msiogope, msifadhaike kabisa; Mimi ndimi niliyekuwa nimekufa na ni hai

tena. Mimi ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Tungemjua Yeye. Na hivyo ndivyo tunavyomjua siku hizi kwa sababu . . .

142 Alitembea siku moja, baada ya ule ufufuo, akishuka barabarani pamoja na marafiki fulani wakienda zao Emau, Kleopa na rafiki yake. Naye akazungumza nao siku nzima, hawakumjua. Lakini alipoingia kwenye jengo usiku huo, katika ile nyumba ndogo ya wageni, wakati alipoketi chini, huku macho yao yamepofushwa kwake, ndipo basi akafanya jambo fulani kama tu alivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwake, na kwa ishara hiyo aliyofanya, vile vile na alivyofanya kabla hajasulubiwa, walitambua ya kwamba ilikuwa ni Yeye, hilo ndilo lililoyafungua macho yao.

143 Sasa, si ni vivyo hivyo siku hizi? Sasa, tuko katika wakati wa mwisho, wakati Yeye alipoahidi ya kwamba huu—kwamba Mzabibu huu utazaa tawi lingine. Yeye aliahidi jambo hilo wakati wa mwisho, na sisi hapa katika wakati wa mwisho. Nitaendea kuchipua kwa tawi hilo asubuhi, Bwana akipenda. Lakini sisi hapa katika wakati wa mwisho pamoja na Yesu yeye yule.

144 Sasa, mmoja atasema, "Jiunge na *hili*," mwingine aseme, "Nenda *huku*," na kadhalika, ungali unapandisha presha, hujui mahali ulipo. Kwa nini usije tu kwenye Kimbilio hilo? Kwa nini usije tu Kwake, uone kama ni kweli? Amini Neno Lake; mwamini Yeye.

145 Huyo hapo Kristo jengoni usiku wa leo. Kristo aliahidi hili: "Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, nitakuwa katikati yao." Hiyo ni kweli? Vema basi, kama hilo si kweli, basi Kitabu hicho kimekosea, kilisema jambo ambalo Yeye hakusema. Lakini sasa, ungewekaje matumaini yako basi, kama Kitabu hicho kilikuwa sahihi? Kama Kitabu hicho ni cha kweli, na kinasema hivyo, basi mkubali Yeye katika Neno Lake, naye Ro—Roho Mtakatifu atathibitisha ya kwamba hiyo ni kweli; hiyo ni: Mungu alisema jambo fulani, Mungu akaja kuthibitisha jambo fulani. Mtu yeyote anaweza kusema analotaka, lakini hilo halilifanyi kuwa sahihi; lakini Mungu anapokuja na kuthibitisha ya kwamba ni kweli, hilo linalifanya sahihi. Amina.

146 Unaamini? Je, uko kwenye Kimbilio hilo? Una haki kwa kila majaliwa aliyo nayo Mungu, kama uko mle ndani. Unaamini hilo? Je, una furaha kuwa katika Kimbilio hili? Je, unaweza tu kuketi na kutoa presha? Sema, "Mungu na ashukuriwe, hatimaye nimefaulu. Nipo hapa kwa neema ya Mungu. Niko katika eneo la usalama, hakuna kinachoweza kunidhuru sasa, nimelindwa na Damu ya Yesu Kristo, kundi la Malaika limenizunguka."

147 "Malaika wa Mungu wamefanya kituo kuwazunguka hao," hawaondoki, wanakaa hapo mchana na usiku, "wamefanya kituo kuwazunguka wamchao." Nawe una Kimbilio. Unaweza kuingia ndani Yake, na kila majaliwa . . . Na ni wakati wa jinsi

gani kuwa katika Kimbilio hili, na kuwa na ushirika pamoja Naye!

148 Ninaamini kama tungemwomba usiku wa leo, kama tungeweza kuwa na ushirika mdogo pamoja na Uwepo Wake, ninaamini angefanya hivyo kwa ajili yetu. Sivyo? Ninaamini angefanya hivyo.

149 Sasa kwako wewe uliyekuwa na shauku hiyo muda mfupi uliopita, ambaye uliinua mkono wako, sijui, usiku wa leo, kama ungeshiriki tu Naye shauku hiyo kwa dakika chache. Kama uko kwenye Kimbilio hilo, unaweza kumgusa Yeye, kwa sababu, Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wako, kama uko kwenye Kimbilio hilo unaweza kufanya hivyo.

150 Sasa, ninaamini jana usiku tulishuka na kusambaza kadi za maombi. Ni wangapi walio wagonjwa hapa, wanaotaka kuombewa? Hebu tuone mikono yenu. Inueni mikono yenu, kila mahali. Loo, tusingeweza kufanyiza mstari bila kadi. Hiyo ni . . . Mnaona? Tusingeweza kufanya hivyo, kwa sababu ingekuwa ni kinyang'anyiro. Lakini hebu—hebu na tusimame kwa dakika moja. Kumbukeni, mtoto huyo mchanga tuliyemwombea hivi punde, katika muda usiozidi saa ishirini na nne Mungu alikuwa amejitokeza jukwaani, mpaka hata akamshangaza daktari huyo. Mnaona? Hakika. Yeye ni Mungu, Yeye huwaponya wagonjwa.

151 Sasa, kama ulijua ya kwamba Yesu alikuwa amesimama moja kwa moja karibu nawe, je, unaamini kama ungemgusa Yeye kwamba angekuponya, kama yule mwanamke alivyofanya aliyekuwa anatokwa na damu? Unaamini hilo?

152 Vema sasa, kama Biblia hapa inatwambia, ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, hebu tuombe tu, na kusema, "Bwana, nimekuja kwenye Kimbilio hili, mimi ni mtumishi Wako, na sasa ninaugua kitu fulani, ama nina kasoro fulani. Naweza kukugusa? Kama ni imani yangu, kama nina imani ya kutosha kukugusa Wewe, basi nijibu. Sasa, Ndugu Branham hanijui, wala simjui, bali Wewe unatujua sote wawili, nami ninaamini ya kwamba Biblia inasema, ya kwamba, 'Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele,' na kama tumebatizwa katika Wewe, na ndani mle Wewe una ofisi za kuliendesha Kanisa Lako kuu kwa ajili ya ukamilifu, kuchukua mashaka yote, mimi nitakuwa tai usiku wa leo, nitaegemea kwenye Mwamba huu, na kuugongagonga mpaka kutokuamini kwote kumeniondokea." Mnaona? "Ninapohisi kutokuamini kote kumekwisha, niungame dhambi zangu zote, niseme, 'Bwana Mungu . . .'"

153 Sasa, unasema, "Ndugu Branham, sivuti sigara, sinywi pombe, sitafuni, sifanyi uzinzi." Hilo—hilo silo. Hayo si dhambi, hayo ni matokeo ya dhambi, hayo ni matokeo ya kutokuamini. Unaona, kama uliamini, usingefanya hayo. Unaona? La, hayo si dhambi. Watu wanaweza . . . Kutokuamini ni dhambi,

"Yeye asiyeamini amekwisha kuhukumiwa." Mnaona? Hayo ni matokeo tu ya kutokuamini.

154 Lakini kama unaweza kuyagongesha hayo yote yakuondokee, useme, "Bwana Mungu, ninaamini yale hasa Neno Lako liliyosema, nami naamini, kama tulivyohubiri jana usiku, ya kwamba kule kuonekana kwa Bwana kunakuja kabla ya kule Kuja kwa Bwana," kwa kuwa ni maneno mawili tu tofauti kabisa. Mnaona? Sasa kule kuonekana, kwa kuwa aliahidi katika siku za mwisho ya kwamba atakuwa pamoja nasi.

155 Na ni Kimbilio la jinsi gani, na ni faraja ya jinsi gani, Wakristo, kwamba tunaweza kusimama hapa usiku wa leo, katika Uwepo wa Mungu, mbele ya Neno Lake, na mambo yasiyowezekana ambayo ameahidi humu ndani, tunaweza kuona yakidhihirishwa moja kwa moja mbele zetu! Ni jambo zuri jinsi gani! Kama hilo si Kimbilio, kama hapo si mahali pa raha, sijui ni mahali gani pangekuwa, kumwona Yesu, Yeye alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Loo, hiyo ni ahadi ya jinsi gani! Sasa, ni wangapi wanaoamini ya kwamba hiyo ni kweli? Vema. Sasa, na tuombe.

156 Baba yetu wa Mbinguni, Wewe ni Mungu. Ninaomba ya kwamba Wewe utatujalia, usiku wa leo, vitu ambavyo watu wanaomba. Nami ninaomba ya kwamba Wewe utajionyesha Mwenyewe hai, kutoa faraja.

157 Muda mfupi uliopita, nilipoomba waaminio wainue mkono wao, Baba, kadiri nilivyoweza kuona, ilikuwa ni asilimia mia moja, kwamba wote walikuwa ni waaminio. Wengi, karibu watu hawa wote siwafahamu, lakini Bwana, Wewe unawajua.

158 Sasa, nimewaambia ya kwamba—ya kwamba kuna Kimbilio, Mnara, Mwa—Mwamba katika nchi yenye uchovu, Mahali katika nchi yenye uchovu sasa, ambapo tunaweza kuja na kuwa salama. Biblia ilisema, "Jina la Bwana ni Ngome imara, wenye haki huikimbilia, wakawa salama."

159 Sasa, kuwahakikishia usalama, Bwana, wakati watu watakapojua ya kwamba si usalama wa kimadhehebu, ni Roho Mtakatifu, usalama wa Damu, ndio tunaoingia ndani yake, jalia hili lijulikane usiku wa leo, Bwana, ya kwamba Wewe ungali ni Yesu, ya kwamba umefufuka katika wafu, kwamba Wewe sasa ni Kuhani Mkuu mashuhuri ambaye anafanya upatanisho kwa—kwa ajili ya chochote tunachoomba.

160 Tunaamini ya kwamba Wewe ulituahidi ya kwamba, "Tukiomba lolote katika Jina Lako litatendeka." Uliahidi jambo hilo, "Kama tungekaa ndani Yako, na ninii yetu . . . na Maneno Yako ndani yetu, ndipo tungeweza kuomba kile tulichokuwa tukitaka, nasi tungepewa."

161 Tunajua ya kwamba Wewe hutimiza ahadi Yako, Bwana. Nami ninaomba ya kwamba Wewe utathibitisha Uwepo Wako,

usiku wa leo. Nasi tunakuomba, Baba, utujalie mambo yale yale yatendeke hapa, usiku wa leo, mbele za watu, kama tu yalivyotendeka kabla ya kusulubiwa Kwako, wapate kujua, baada ya miaka elfu mbili, ya kwamba Yesu hajapata umri wa siku moja zaidi, Yeye ni Kristo yeye yule aliyekuwa daima, Yeye hawezi kushindwa wala kubadilika kamwe.

162 Ninaomba ya kwamba utawapa faraja. Basi ujalie usiku wa leo, Baba, kwamba wao wakijua ya kwamba sisi ni wanadamu tu, na mambo haya yasingewezekana kwa mwanadamu kuyafanya, bali Mungu aliahidi kufanya hivyo kwa Kanisa La—Lake, watu Wake walioitwa watoke, wale waliokuwa chini ya ile Damu. Tujalie, Baba.

163 Na kama kuna wengine hapa ndani, usiku wa leo, ambao hawako chini ya Damu, jalia upesi na kwa utamu, jalia waombee majaliwa hayo, nami nina hakika watapewa. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

164 Sasa, enyi kanisa, ninyi mnaosafiri, sizungumzi juu ya madhehebu, ninazungumza juu yenu ninyi watu katika madhehebu, ambao ni Kanisa, ninaomba jambo hili, ya kwamba kuna mtu anayeweza kuja na kusema lolote analotaka kusema, lakini isipokuwa litoke kwenye Biblia, kidogo ningekuwa na shaka nalo.

165 Sasa, Mungu anaweza kufanya chochote anachotaka kufanya, Yeye ni Mungu, mimi si mtu wa kusema kwamba Yeye hafanyi. Yeye hushughulikia shughuli Zake Mwenyewe, hata siwezi kushughulikia zangu, bali ninamtegemea Yeye.

166 Lakini vipi kama Yeye akiahidi, na ni ishara ya Biblia? Kama vile, "Katika Jina Langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya. Wakishika nyoka, au kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya. Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena; bali ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi," kiwakilishi nafsi, "nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Na kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Hizo ni ishara za Biblia, rafiki. Hao ni waaminio waliopita kutoka mautini kuingia Uzimani.

167 Biblia inasema ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Sasa, kama una udhaifu usiku wa leo, ama unamjua mtu aliye na udhaifu usiku wa leo, ukiomba tu na kumwamini Mungu, kama ukiomba tu sasa hivi, ninaamini Mungu, kwa Roho Wake Mtakatifu katikati yetu hapa . . .

168 Sasa, enyi marafiki, tumeona hili, wengi wenu mliona likitendeka, lakini shida ya Wamarekani, tumeliona kupita kiasi, ni la kawaida sana kwetu sasa.

169 Mzee baharia mmoja alikuwa akija kutoka baharini siku moja, naye akakutana na mtu akishuka, mshairi aliyekuwa ameandika juu ya bahari, lakini hakuwa amewahi kuiona, naye akasema, "Unaenda wapi, mtu wangu mwema?"

170 Akasema, "Ninaenda baharini." Kasema, "Loo, nimeandika habari zake, yale niliyosoma." Kasema, "Sasa, nitajua habari zake." Akasema, "Ninashuka kwenda kuiona. Nimeninii . . . Loo, jinsi moyo wangu unavyosisimkwa!" Akasema, "Ninataka kusikia harufu ya mawimbi yake yenye chumvi, ninataka kuona ikipita na kurusha mawimbi hewani, ninataka kuwasikia shakwe wakipiga makelele, na kuona mbingu za samawati zikijiakisi katika maji yake, katika mawimbi yake meupe huku ikichezacheza." Alikuwa mshairi, kwa hiyo angeweza kweli kulielezea.

171 Ndipo yule baharia mzee akasema, "Sioni kitu kinachosisimua sana kuihusu," kasema, "Nilizaliwa juu yake, zaidi ya miaka arobaini iliyopita." Mnaona, alikuwa ameiona sana, hata ikawa ni kawaida kwake.

172 Hiyo ndiyo shida ya watu wa Full Gospel, lakini saa inakuja hivi karibuni ambapo mtalililia, na halafu hamtaliona. Hebu kamwe lisichakae kwenu, msiache Roho Mtakatifu achakae kwenu, jalia daima awe safi na mpya.

173 Jalia kila tendo la Mungu liichangamshe nafsi yangu. Ninashangaa kila usiku, kila siku, ninapotembea na kumwona Yeye akisema mambo, na kuliona likitendeka jinsi tu Yeye alivyosema litatukia, jinsi ambavyo Yeye atalitabiri miezi kadhaa kabla halijatimia, kisha unaliona vizuri kabisa, hata yodi moja haikosei.

174 Neno Lake haliwezi kushindwa, Yeye ni Mungu. Na hilo ni kimbilio la jinsi gani! Ni faraja ya jinsi gani kujua ya kwamba sisi si watoto wa kuyumbishwa tu, bila kujua tunakoelekea, tunajua tunakoelekea, Mungu aliahidi jambo hilo, Yeye huthibitisha ahadi Zake.

175 Basi huenda watu wakakwambia ya kwamba tunashikwa na mihemuko kupita kiasi, si mhemuko, bila shaka, huo, kwa njia moja ni mhemuko. Lakini chochote ambacho hakina mhemuko kimekufa, kwa hiyo kama dini yako haina mhemuko kidogo juu yake, afadhali uizike, maana i—imekufa. Kwa hiyo hakika linasisimua.

176 Wakati Yesu alipoingia, Yerusalemu, watu walipiga mayowe na kupaza sauti mpaka watu wakasema, "Wafanye wanyamaze."

177 Akasema, "Wakinyamaza, miamba itapiga kelele mara moja." Mwana wa Mungu alikuwa njiani, na kitu fulani hakina budi kutokea katika Uwepo Wake.

178 Sasa, Mwana wa Mungu yupo hapa usiku wa leo, ninaamini hilo. Mimi si Mwana wa Mungu, mimi ni mwana wa Mungu

aliyepewa mamlaka, kama ulivyo wewe, mimi ni sehemu ya Roho Wake. Na ikiwa Roho Wake yu ndani yangu. . .Kama niliwaambia nilikuwa na roho ya John Dillinger, mngenitarajia kuwa na bunduki, na niwe mhalifu. Kama niliwaambia roho ya msanii ilikuwa ndani yangu, mnatarajia nizichore hizo picha. Kama niliwambia roho ya askari fulani mashuhuri, mnatarajia nijue silaha zote na kila kitu, maana roho yake iko ndani yangu. Kama nikiwaambia Roho wa Kristo yuko ndani yangu, basi ninapaswa kufanya kazi za Kristo, niishi aina ya Maisha aliyoishi, Maisha yaliyotolewa sadaka kwa ajili ya watu, hiyo ni kweli.

179 Ninawazia juu ya wakati ambapo nabii aliwaendea watu, wakati walipotaka kujifanya kama watu wengine. Hapo ndipo walipofanyia kosa la kusikitisha, walipotaka mfalme, walitaka kutenda kama watu wengine. Ni vibaya sana kwamba tuliwahi kuweka madhehebu katika Pentekoste, tukivunja vizuizi, na kadhalika, ni vibaya sana, ilimkatilia mbali jamaa huyo mwingine. Wala hatupaswi kutaka kutenda kama makanisa mengine, sisi ni kundi la watu waliozaliwa mara ya pili, tuko huru. Hatujafungwa na kanuni za imani za mtu yeyote, tuko huru katika Kristo.

180 Sasa, lakini ilikuwa ni vibaya sana walifanya hivyo, bali tungali tuko huru kwa neema ya Mungu, na Yeye yuko pamoja nasi usiku wa leo. Haitupasi kuyumbishwa huku na huku, tukisema, "Inakubidi kufanya *hiki*, na huna budi kufanya *kile*, na kufanya *kile*," tunamwona tu Kristo akija miongoni mwetu. Na ni faraja ya jinsi gani kumwona Kristo yeye yule aliyeahidi, "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata mwisho wa safari, mwisho wa ulimwengu," na kushuka moja kwa moja na kujithibitisha Mwenyewe miongoni mwetu (Hilo si ni zuri sana?), akijifanya Mwenyewe yule yule jana, leo, na hata milele.

181 Hakuna watu wengi hapa ndani ninaowajua. Ninyi wagonjwa, ama ninyi mlio na shauku moyoni mwenu, na unajua ya kwamba sikujui, wala kujua shauku yako, inua mkono wako. Vema, ni kila mahali. Vema. Sina mamlaka juu ya hii, inanitawala mimi. Lakini kama ingetokea ije juu ya mtu anayenijua, na mtu fulani ambaye nimekutana naye au kitu fulani, nami ninawajua, nao wanatoka Jeffersonville ama mahali fulani, basi mseme.

182 Lakini nataka kuwaulizeni jambo fulani. Wakati Bwana wetu Yesu aliposimama hapa duniani na kuwaangalia wasikilizaji Wake, maskini mwanamke mmoja aligusa vazi Lake siku moja, ndipo akageuka na kusema, "Ni nani aliyenigusa?" Hakujua alikuwa ni nani, maskini huyo mwanamke huenda alikuwa ameketi chini, kama m—mlivyo huko nje, na Yeye alifanya nini? Alisema. . .Akampata. Mnaona, Yeye ali-. . . asingeweza kufichika, Naye akasema, "Imani yako imekuokoa." Akamwambia, kutokwa kwake na damu kulikuwa kumekoma,

kwa sababu alikuwa amemgusa. Sasa, alifanya hivyo yeye mwenyewe. Sasa, Biblia ilisema ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.

183 Wakati Mtakatifu Petro alipomjia, mzee mvuvi fidhuli tu, wao . . . tunaambiwa hata hakuwa na elimu ya kutosha kuandika jina lake mwenyewe, bali hata hivyo ilimpendeza Mungu kumpa funguo za Ufalme, hiyo ni kweli, kwa sababu ya imani yake. Alikuwa na ufunuo ya kwamba Yeye alikuwa ni Nani, alisema, "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu."

184 Sasa, Yesu hajafa, Yeye yu hai, Kuhani Mkuu. Na kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, kama ulimgusa Yeye, Yeye angetenda vivyo hivyo. Hiyo ni kweli? Sasa, Yeye aliahidi mambo haya yatafanywa.

185 Ninaamini katika Biblia, ninaamini ya kwamba Hiyo ni Neno kamili la Mungu. Siamini inatubidi kutoka kwenye Biblia hiyo tupate chochote, ya kwamba kila ahadi ya Kiungu iko humo ndani. Ninaiamini kwa moyo wangu wote, nafsi yangu yote, nguvu zangu zote, na yote yaliyo ndani yangu, ninaiamini. Huenda nisiwe na imani ya kutosha kufanya kila ahadi itimie, ila hakika sitasimama njiani mwa wale walio na imani, wanaoiamini. Ninawatakeni mliamini kwa yote yaliyo ndani yenu.

186 Sasa, kila mtu, kama Kristo atakuja miongoni mwetu kwa Roho Mtakatifu, na atawafanya . . . Ninyi ni watoto Wake, bloku zilizoko Hekaluni. Mnajua siku hizi tunasikia mengi sana kuhusu, kama tu ilivyokuwa katika siku za mwanzoni, kuna ufuasi mwingi sana, "Hatuna budi kuwavutia wafuasi *kadha*."

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . Neno, kuwa wana na binti za Mungu. Jambo ndilo hilo. Tunahitaji uashi wa Roho Mtakatifu wa Mungu.

187 Biblia inasema ya kwamba "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili," Waebrania 4:12. "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili." Sikilizeni, Neno, ni wangapi wanaoamini ya kwamba hapo mwanzo kulikuwako Neno? Hiyo ni kusema, kwanza Hilo lilikuwa ni wazo, na halina budi kuwa ni wazo, basi, linapotamkwa, linakuwa Neno. Na halafu, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu," alipolinena, "naye Neno akafanyika mwili akakaa kwetu."

188 Sasa, huyo alikuwa ni Yesu, wakati alipokuwa hapa duniani, aliyatambua mawazo ya watu, hilo ndilo lililowafanya waaminio wote wa kweli wajue ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Nabii ambaye Musa alikuwa amenena habari zake, angeinuliwa. Hawakuwa na nabii kwa mamia ya miaka.

189 Ninaamini wakati umewadia tena, ambapo, Biblia inaahidi ya kwamba katika siku za mwisho, Roho huyo atakuja juu ya nchi, na atairudisha imani ya watoto iwarudie baba wa

Kipentekoste tena, iirudie ile imani asili. Ninaamini ni Nuru za jioni. Ninaamini ya kwamba iko hapa.

190 Ninaamini huyo Roho wa Mungu, huyo Kristo, yupo hapa usiku wa leo. Nami ninawaomba, kama rafiki yangu, na ndugu yangu na dada, aminini ya kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yupo hapa. Na unapoamini hilo, mguse kwa udhaifu wako, kwa imani yako kuliamini, na kusema, "Bwana Mungu, kama mtu huyo, yeye hanijui mimi, simjui, yeye hanijui, lakini kama ameniambia kweli, basi jalia Roho Wako anene kupitia midomo yake, na unijalie nikuguse, Nawe ulithibitishe kwa midomo yake."

191 Kama yule mwanamke alivyofanya wakati alipogusa upindo wa vazi Lake katika siku hizo, wewe gusa vazi Lake, kwa kuwa Yeye anaweza kuguswa na imani yako, kama yule mwanamke, labda si kimwili, bali kama yule mwanamke. Je, ingewafanya mwe na furaha na kushangilia katika Kimbilio kama mngeninii . . . kama mngeweza, mngemwona Yeye akifanya hivyo? Inueni mikono yenu kama mnaamini Yeye angefanya hivyo. Asanteni.

192 Sasa, Baba, hilo tu ndilo ninalojua kusema. Ninajaribu kuwaambia juu ya Mahali pa salama ambapo wanaweza tu kupumzika, na, Mungu, Humu ndani kuna uponyaji, Humu ndani kuna Mwamba ambao kutokuamini kwote kunaweza kupondwa na kuondolewa kwanye huo, Mwamba wa Neno. Na jalia Neno lije mbele sasa na lifanyike mwili miongoni mwetu. Nalo lilisema, "Ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, huchoma hata kugawanya, na Mtambuzi wa mawazo ya moyo," Mtambuzi wa mawazo ya moyo.

193 "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, basi ombeni mtakalo." Bwana, nimetolewa nje, nikakanyagwa, nimepondwapondwa, bali nimejaribu kusimama mwaminifu, nina furaha kufanya hivyo kwa Neno Lako, jalia likae daima moyoni mwangu. Na mbele ya kusanyiko hili usiku wa leo, ambapo nitasimama tena, siku moja, kama si duniani tena, kwenye Siku ya ile Siku kuu wakati Yesu atakapokuja, nina ninii . . . najua ya kwamba Neno Lako ni Kweli.

194 Nisaidie, Ee Bwana, ili niweze kutumika usiku wa leo. Na kama . . . Ninajua mimi si mwanatheolojia, Baba, kamwe hukuniitia jambo hilo, bali ninaomba ya kwamba Wewe utairuhusu huduma uliyonipa kuwabariki watu kwayo, ijitokeze sasa. Katika Jina la Yesu Kristo, naomba Neno lije, na kupenya ndani *hapa*, na kuyatambua mawazo ya moyo, kusudi watu wapate kujua ya kwamba Neno la Mungu linakaa ndani yetu. Katika Jina la Yesu, ninaomba, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Amina.

195 Angalieni huku, sasa, ninasema jambo hili kama Petro na Yohana, waliopitia kwenye lile lango Zuri, alisema, "Tutazame."

Hivyo ndivyo ninavyowaomba mfanye, mwangalie huku, sio kuniangalia mimi, bali yale nimesema. Lolote ulilo na shauku nalo moyoni mwako, wewe amini ya kwamba Mungu atakupa. Sema, "Bwana Yesu, jalia nikuguse."

196 Ni wangapi kwenye jengo hili wamewahi kuona picha ya ile Nuru, yule Malaika wa Bwana, ile inayoning'inia hapa Washington? Mimi ni ndugu yenu, ile Nuru, kama mnaweza kuiona, inaning'inia si futi mbili kutoka kwangu sasa hivi. Aminini tu. Kama hamwezi kuiona, mnaona, ombeni, mwone kama Mungu hatathibitisha. Nuru hiyo, kama hiyo Nuru ndiyo Nuru ile ile iliyokutana na Paulo akienda zake Dameski (Yeye alisema, "Mimi ni Yesu," Yeye alikuwa amerudi akawa ni Mungu, akawa ni Roho, Neno lilifanyika mwili, akarudi kwenye Neno.), kama Hiyo ni Nuru ile ile, italeta Uhai wa namna ile ile, tendo lile lile. Mnaiona?

197 Mama huyu aliyeketi papa hapa, hivi hatufahamiani, mama? Sikujui, sijawahi kukuona. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Unaamini Maneno ambayo nimehubiri ni kweli? Nasi hatufahamiani kabisa, wewe ni ninii tu, nijuavyo mimi, mwanamke ambaye ameingia, akaketi hapa chini. Lakini ulikuwa ukiamini kwa ajili ya jambo fulani, unajaribu kupata kitu fulani kutoka kwa Mungu. Na kama mimi ni mtumishi wa Mungu, na nimesema kweli ya Mungu, nalo Neno la Mungu na kweli linakaa *humu* ndani, litajizaa Lenyewe, litaitangaza. Utajua kama ni kweli ama si kweli.

198 Unamwombea mtu fulani, ni mtoto wako, ni huyo msichana mdogo aliyeketi papo hapo. Naye maskini msichana huyo, unaamini Yeye ataniambia shida yake? Ingekusaidia? Ana ugonjwa wa moyo. Laiti ungeamini kwa moyo wako wote, na ushuke uende pale na kuweka mikono yako juu ya mtoto huyo! Shuka uende pale, uweke mikono yako juu ya huyo mtoto.

199 Tumbo la uzazi lililomzaa kwa dunia hii, mkono wa huyo mama umewekwa juu ya huyo mtoto, Bwana, kama alikuwa na imani ya kutosha kugusa vazi Lako, basi ninakuja na Upanga wa Mungu kwa Neno la Mungu kufanya upasuaji.

200 Toka, Shetani, ninakukatilia mbali kwa Neno la Mungu, la ahadi, kwamba ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Mwache huyo msichana, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Unaamini ataishi, na kupata afya? Kama ulivyoamini, ndivyo itakavyokuwa.

201 Sasa, ninamwomba mtu fulani amhoji huyo mwanamke, amwulize kama kila Neno lililosemwa ni kweli. Simjui huyo mwanamke, sijawahi kumwona, sijui lolote kumhusu, lakini yale yaliyosemwa ni kweli.

202 Vipi kuhusu mtu anayepitia hapa? Vipi kuhusu wewe kuamini? Hebu tuchukue angalau wawili ama watatu kwa ajili

ya ushahidi. Nina furaha kuwa katika Kimbilio hili, niko salama milele. Nampenda. Jinsi ilivyo tamu kumtumaini Yesu!

203 Ni changamoto jinsi gani kwa watu! Aliahidi, "Itakuwa Nuru wakati wa jioni. Kutakuwako na siku ambayo haitakuwa mchana wala usiku." Imekuwa si—siku ya utusitusi, wa kutosha tu kutembea na kukubali. "Lakini wakati wa jioni itakuwa Nuru."

204 Maskini mama, unatambua tu kadiri uwezavyo kwamba jambo fulani limetukia, ninaiangalia moja kwa moja, hiyo Nuru ilikaa moja kwa moja juu yako, ninaiangalia. Sijawahi kukuona hapo kabla, nadhani hatufahamiani. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

205 Kuna kivuli cheusi kilichokuzunguka, ni kivuli cha mauti. Unaugua u—uvimbe, na uvimbe huo uko kwenye titi lako, matiti yote mawili. Asilimia kubwa ya matiti yako imefunikwa na uvimbe. Una tumaini moja: kwamba una imani ya kutosha kumgusa Yeye kufanya jambo kama hilo. Wewe ni mtu mzuri, nina mawasiliano mazuri ya Roho pamoja nawe. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Unajua sikujui, nawe unajua hili, unajua ya kwamba hisi tamu sana imekuzunguka kila mahali, hiyo ni ile Nuru, ule mwako wa Nuru.

206 Hutoki hapa, umetoka mbali na hapa, Birmingham. Ninaona lile soko la ndizi kule. Jina lako ni Binti Vincent, hiyo ni kweli. Mwamini Mungu. Sasa, kwenye wakati huu, mama, kimekuacha, kile kivuli kilichokuwa juu yako kimeondoka. Sasa, usiwe na shaka, utapona.

207 Ninamwomba mtu yeyote aje kumhoji huyu mwanamke, apate kujua. Kama kungekuwako na daktari, kwa nini usije ukamwulize, na kuchunguza? Una shaka kidogo. Ambayo, ninajua ipo, kwa hiyo—kwa hiyo kwa nini nisiliseme? Nilikuwa nikilifichua hilo, lakini linaumiza hisia nyingi kupita kiasi.

208 Vipi kuhusu mtu fulani *hapa* ndani? Baadhi yenu huko nyuma mahali fulani, iweni na imani. Siwezi kufanya hili, wewe lifanye. Ninajaribu tu kumwakilisha, kumwakisi, kama kwenye kioo, kwenu, nikiyafanya maisha yangu kuwa kioo Chake, apate kujiakisi Mwenyewe. Mnajua siyajui mambo haya, wala nisingeweza kuyafanya. Ninaninii tu . . . Ninyi iweni tu na imani, wala msitie shaka, aminini.

209 Papa hapa nyuma, ni mwanamume, iko juu ya mwanamume. Anasumbuliwa na hali ya wasiwasi, natumaini hataukosa. Anatoka Pennsylvania. Mungu, nisaidie. Bw. Carnes, simama kwa miguu yako. Mimi ni mgeni kwako, sikujui. Mambo hayo ni kweli, inua mkono wako. Nenda nyumbani, umepona. Yesu Kristo amekuponya.

Mnamwamini Mungu? Aminini pia kwamba nimewaambia ukweli kuhusu Yesu Kristo, Uwepo Wake.

210 Ninaamini hizo ni safu tatu. Tuna nini, moja zaidi? Hebu twendeni *hapa*. Vipi kuhusu baadhi yenu *hapo* ndani. Mtaamini? Ni wangapi wanaoteseka, wanaohitaji msaada kutoka kwa Mungu, nawe unaamini ya kwamba . . . wala hujui . . . unajua ya kwamba sijui hali yako, inua mkono wako, useme, "Ni mimi, ni—ninaamini." Kila mahali tu. Aminini sasa.

211 Maskini jamaa huyu anayeketi hapa ameinua mkono wake, hukujua ulikuwa na imani kiasi hicho, sivyo? Kama una imani ya kutosha, katika hali yako, kumwita Mungu jukwaani, kamwe usinywe tone lingine la wiski maadamu ungali hai, wala kamwe usivute sigara nyingine, mwamini Mungu, nawe utaponywa. Utalikubali? Utaamini? Vema, basi nenda, na Mungu akupe afya.

212 Hebu tuseme, "Bwana asifiwe." Mnaamini Yeye yupo hapa? Ni wangapi wenu wangetaka kukiri kutokuamini kwenu na wangetaka kusema, "Mungu, unirehemu," katika Uwepo wa Roho Mtakatifu? "Ninajua ya kwamba hakuna mtu duniani angeweza kufanya mambo hayo. Unirehemu." Ungama makosa yako, mwambie Mungu, "Nime—nimekuwa asiyejali, Bwana. Sasa nataka kuingia katika ushirika huu mkuu, ninataka kuingia katika Kimbilio hili. Nitakuamini kwa moyo wangu wote." Inua mkono wako na useme, "Mungu, ni mimi, ni mimi, ni—niko kwenye mwisho wa safari, na—nataka kufanywa sawa." Unaamini hilo? Ungama dhambi zako sasa. Na tuombe. Kila mmoja wenu aombe kwa njia yako mwenyewe.

213 Bwana Yesu, sisi ni wanadamu, Bwana, tuko tayari kuungama dhambi zetu. Ninakiri dhambi za watu hawa, ninakiri dhambi zangu mwenyewe, tumekosa kuamini kupita kiasi, Bwana. Majira yanaingia giza, Mwana wa Mungu yu karibu kuwasili pamoja na . . . Nami naomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba Wewe utatusamehe dhambi zetu. Bwana, ninaomba ya kwamba Roho Mtakatifu sasa atatuondolea kila kutokuamini.

214 Loo, laiti angaliweza tu kuingia moyoni mwetu, kungekuwako na Siku nyingine ya Pentekoste, kungekuwa na ha—hali kama hiyo katika kanisa hili, na kundi hili la watu usiku wa leo, mpaka ingetangazwa kote nchini ifikapo asubuhi.

215 Roho Mtakatifu, vunja kila kizuizi cha dhambi. Jalia apite kama ndege kupita kizuizi cha dhambi, na kutikisa kila pingu za kutokuamini. Jalia kila tai agongeshe kichwa chake kwenye ule Mwamba wa Miaka mpaka Roho Mtakatifu atakapochukua mamlaka kamili.

Shetani, umepotea, umeshindwa vita na, katika Jina la Yesu Kristo, liache kusanyiko hili, toka ndani yao, kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

216 Sasa kwa kuwa umekiri dhambi zako, sasa kwa kuwa unaamini, je, unaamini ya kwamba umeondoa kila pingu ya ufahamu wako, kwamba hakuna kitu kinachokuzuia, hakuna kitu kimoja njiani mwako, bali unaamini uko huru? Unaamini

ya kwamba kutokuamini kwote kumekuacha? Unaamini ya kwamba sasa uko katika kimbilio hilo la raha? Unaacha presha yote: "Je, nitaponywa? Naweza kuponywa?" Tayari umeponywa.

217 "Ndugu Branham, kama utaniwekea mikono yako. . . " Mikono yangu haina uhusiano wowote nalo, ni mkono Wake. Kama wewe ni mwenye dhambi, tayari umeokoka, amini tu, na ulikubali, na kulitekeleza. Kama wewe ni mgonjwa, tayari umeponywa.

218 Hivi Mungu angesimama hapa na kufanya jambo kama hilo, na kumwacha mnafiki, ambaye ni mtu asiyejua wanalozungumzia, aje hapa na ange—angemthibitisha mwo—mwongo, angemthibitisha mnafiki? Mungu hashughuliki na wenye dhambi, Mungu hushughulika na Kweli, nalo Neno Lake ni Kweli, nami nimewaambia Kweli.

219 Pia, enyi marafiki, ninasema, usiku wa leo, kama mtaamini yale niliyowaambia, hakutakuwako na mtu mnyonge miongoni mwetu. Kila mmoja wenu ameponywa, kwa kupigwa Kwake tayari mmeponywa. "Kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Mnaamini hilo?

220 Sasa, ninyi mnaoamini katika kuwekea mikono, mlioinua mikono yenu mlikuwa waaminio, basi weka mkono wako juu ya mtu fulani aliye mbele yako humo kitini. Weka mkono wako hapo, unataka. . .

221 Biblia haisemi, "mikono ya William Branham," Biblia haisemi, "mikono ya Oral Roberts," Biblia ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na *hao* waaminio, *wakiweka* mikono *yao* juu ya wagonjwa, watapata afya." Sasa, ninyi ombeni, ombeni, ungameni; ungameni mumekosea. Mwambie Mungu kwamba unamwamini, na unaweza, kila mmoja, kufanywa mzima kabisa saa hii. Aminini. Haleluya! (. . .?. . .)

Ishikilie, usiiachilie. Dumu nayo, ni ahadi, Mungu alisema hivyo. Usiyumbishwe na kila kitu, amini sasa hivi.

222 Ninakupenda, wewe ni rafiki yangu, sijaribu kukuzungumzia kwa ujeuri, bali ni—ninasema jambo hilo, sina budi kulishikiza la sivyo Shetani atawanyakua kutoka kwake, kutoka kwenye onyesho hili kuu la Uwepo wa Roho Mtakatifu hapa usiku wa leo. Bila shaka hata kidogo, Biblia inashuhudia yale Mungu aliyosema yangetukia, kuna Upepo wenye nguvu uendao kasi ukijaribu kuingia kwenye hili kusanyiko, na kujaza kila nafsi hapa kwa Uwepo wa Mungu; usimwache Shetani akunyang'anye, ushikilie, mpaka utakapovuka kizuizi cha kutokuamini. Amina.

223 Sijali jinsi ulivyolemaa, jinsi ulivyo mgonjwa, wewe ni nani, ama unakotoka, ninakupa changamoto, katika Jina la Yesu Kristo, kama ulimaanisha hilo kutoka moyoni mwako, simama kwa miguu yako na ulikubali. Haidhuru wewe ni nani, kile ulicho, simama. Jambo ndilo hilo, inuka, hiyo ndiyo njia. Amina.

Simameni kila mahali. Haya basi, kusanyiko zima kamili kila mahali.

*Imani Yangu Inakutazamia.*

. . . imani inakutazamia,
Ewe Mwana-Kondoo wa Kalvari,
Loo, Mwokozi . . .

Na tuinue mikono yetu sasa na kumwimbia.

. . . Mungu;
Sasa nisikie ninapoomba,
Ondolea mbali hofu yangu yote,
Ee nijalie tangu leo
Niwe Wako kabisa!

62-0609E Kutoa Presha
Aberdeen High School
Aberdeen, North Carolina Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org